SUPA JACKPOT
TZS. 1,063,605,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## DADA wa kazi kortini madai kunyonga bosi kwa mtandio


Royal Tour iwe ni kazi endelevu, isisubiri matukio ndio tunaibuka
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
RC Mrindoko: Katavi tunafunguka kwa kasi kona zote, barabara na madaraja
Rais Ruto aweka wazi mtaji wa serikali, amtetea binti yake

UKURASA 13

Nipashe
Ijumaa Januari 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581182
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Saa 43 za uteuzi wa Diwani Ikulu

UKURASA 2



Jeneza la Papa Mstaafu Benedict XV1, likiwa limebebwa ndani ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, Rome, Italia. atazikwa katika kaburi la zamani la Papa Yohane Paulo II chini ya kanisa hilo. **PICHA: MTANDAO**

## Rukhsa mikutano ya kisiasa yaibua wanasheria na wadau

UKURASA 4

## Wafanyabiashara walia na utitiri wa kodi nchini

UKURASA 2

**MICHEZO** ROBERTINHO AWAPA 'TANO' MKUDE, KIBU UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura (kushoto), akipokea Katiba ya Watendaji wa Mtandao wa Polisi Wanawake nchini (TPF-NET) kwa Mwenyekiti wa Mtandao huo ambaye ni Kamishna wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, CP Susan Kaganda, baada ya ufunguzi wa kikao kazi cha watendaji wa mtandao kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Saa 43 uteuzi wa Diwani Ikulu

**Na Christina Mwakangale**

NI rekodi mpya ndani ya Ikulu. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na mteule wa Rais kukaa ndani ya uteuzi kwa saa 43 na dakika 25 tangu kuteuliwa hadi kutenguliwa tena kabla ya kuapishwa kushika wadhifa aliopewa.

Hilo limetokea kwa Kamishna wa Polisi (CP) Diwani Athumani Msuya, ambaye Januari 3, mwaka huu, aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ikulu na kisha jana mchana, kutolewa taarifa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi huo.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alitoa taarifa kupitia televisheni kwamba amefanya mabadiliko ya nafasi za uongozi katika serikali, akiwa Ikulu jijini Dar es Salaam.

Katika mabadiliko hayo, Rais Samia alitangaza kuwa amemteua Diwani kuwa Katibu Mkuu, Ikulu akichukua nafasi ya Dk. Moses Kusiluka ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Dk. Kusiluka alichukua nafasi ya Balozi Hussein Kattanga, aliyeteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania, New York nchini Marekani na Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa (UN) wenye makao makuu jijini New York.

Kabla ya uteuzi huo, Kamishna Diwani alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) ambayo kwa sasa imechukuliwa na Said Hussein Masoro, ambaye kabla alikuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Masuala ya Ndani wa TISS.

Licha ya Diwani kutenguliwa kabla ya kuapishwa kushika wadhifa mpya, Rais Samia pia aliwahi kufanya uteuzi wa Azza Hillal Hamad, aliyewahi kuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga kupitia CCM na kutengua kabla ya kumwapisha.

Hamad alitangazwa Mei 29, 2021 kuwa ameteuliwa na Rais Samia kuwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Simiyu katika mabadiliko makubwa ya makatibu tawala wa mikoa. Hata hivyo, taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu iliyotolewa Mei 31, 2021 ilitangaza kuwa Rais ametengua uteuzi huo na atapangiwa majukumu mengine.

**BASHIRU MUDA MFUPI**

Wakati hayo yakitokea, kumbukumbu zinaonyesha kuwa viongozi wakuu na waandamizi walioteuliwa kushika nyadhifa Ikulu, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, alikuwa na rekodi ya kukaa muda mfupi katika nafasi hiyo kuliko watangulizi wake.

Balozi Dk. Bashiru ambaye kabla ya wadhifa huo alikuwa Katibu Mkuu wa CCM, aliteuliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, Februari 26, 2021 kuchua nafasi ya Balozi Mhandisi John Kijazi, ambaye alifariki dunia.

Dk. Bashiru aliondolewa kwenye nafasi hiyo Machi 31, 2021 baada ya Rais kumteua Balozi Kattanga ambaye awali alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Japan. Baada ya kuondolewa katika nafasi hiyo, aliteuliwa kuwa Mbunge katika nafasi 10 za kuteuliwa na Rais.

**DIWANI NI NANI?**

Kamishna Diwani, ambaye ni kachero mwandamizi, kwa muda mrefu alikuwa akijulikana kuwa ni ofisa wa polisi kutokana na nyadhifa mbalimbali alizokuwa ameshika ndani ya Jeshi la Polisi.

CP Diwani ndani ya jeshi hilo ameshika nafasi mbalimbali tangu akiwa ofisa wa ngazi za chini na alipanda ngazi mbalimbali hadi alipoteuliwa kuwa Kamanda wa Polisi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mbeya na Shinyanga.

Baadaye alirejeshwa makao makuu ya polisi katika Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (CID) na baadaye kuwa Naibu Mkurugenzi wa Idara na wakati huo huo akikaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) iliyokuwa ikishikiliwa na Kamishna Robert Manumba.

Mei 12, 2015 aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, alimteua Diwani kuwa DCI akichukua nafasi ya Manumba ambaye alistaafu utumishi ndani ya Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, uteuzi wake katika nafasi hiyo ulitenguliwa na Dk. Magufuli Oktoba 29, 2016 na wiki tatu baadaye (Novemba 18, 2016), aliteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Kagera.

Septemba 6, 2018 ilibainika kuwa ni miongoni mwa maofisa waandamizi wa TISS baada ya Rais (Hayati) Magufuli kubainisha hayo alipomteua kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, akichukua nafasi ya Kamishna wa Polisi (CP) Valentino Mlowola alyeteuliwa kuwa Balozi.

Nyota ya Diwani ambayo ilionekana kufifia baada ya kutenguliwa nafasi ya DCI, iliendelea kung'ara zaidi baada ya Septemba 12, 2019 kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu TISS kuchukua nafasi ya Dk. Modestus Kipilimba, aliyeteuliwa kuwa Balozi. Amedumu katika nafasi hiyo hadi Januari 3, 2022 alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu Ikulu, nafasi ambayo hakuitumikia kutokana na kutenguliwa kabla ya kuapishwa.

Uteuzi wake kwa nafasi hiyo mpya ulitangazwa Jumanne saa 2:06 usiku na jana saa 9:19 alasiri taarifa ikatolewa kuwa ametenguliwa, kwa mujibu wa ukurasa wa Twitter Ikulu. "Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, ametengua uteuzi wa Kamishna Diwani Athumani Msuya, aliyemteua tarehe 03 Januari, 2023 kuwa Katibu Mkuu Ikulu." ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, Rais Samia pia alimteua Mululi Majula Mahendeka, kuwa Katibu Mkuu Ikulu. Mahendeka alikuwa Ofisa Mwandamizi wa Ofisi ya Rais, Ikulu.

# Wafanyabiashara walia na utitiri kodi serikalini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA mkoani Njombe wamelalamika kushindwa kutatuliwa kwa kero mbalimbali za kibiashara zikiwamo sheria kandamizi na utitiri wa kodi ambazo zimekuwa kikwazo kwao.

Waliwasilisha hoja yao hiyo wakati wa Mkutano wa Saba wa Baraza la Wafanyabiashara Mkoa wa Njombe uliohudhuriwa na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji.

Wafanyabiashara hao, akiwamo Edward Kazimoto, walisema ukadiriaji kodi ni mbaya, sheria kandamizi za biashara pamoja na ubabe katika ukusanyaji kodi ni kikwazo kwa maendeleo ya biashara nchini.

"Ukadiriaji wa kodi ni mbaya sana, unakuta biashara imeshuka hufanyi kama mwanzo lakini watu wa TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) wakija, wanakukadiria vilevile," alilalama Kazimoto.

Ushuru kwenye biashara ya mbao ulionekana kuvuta hisia za wafanyabiashara wengi mkoani Njombe wakizinyooshea kidole mamlaka kwa kutofautiana katika kuitoza.

Sebastian Msigwa alisema utozaji wa ushuru kwenye mbao umekuwa kero kubwa, akifafanua kwa kauli: "Kutokana na changamoto ya kutoeleweka kwa ushuru kwenye mbao, halmashauri zinatoza Sh. 150 kwa ubao, mara muhuri wa moto na ukihoji hupati majibu ya kueleweka, sasa hivi tumeamua kuachana na biashara ya mbao, tunakata miti ili tupande parachichi," alisema Msigwa.

Tony Chaula alilalamikia halmashauri kutoza Sh. 3,000 kwa kila mfanyabiashara pasi na kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu makato hayo.

Katika mkutano huo, Waziri Dk. Ashatu aliwataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kusimamia sheria za nchi hususani sheria inayotoza ushuru wa mbao kwa asilimia tatu na si vinginevyo.

"Kama nilivyosema, kodi hukusanywa na sheria, huwezi ukaamka ukasema 'hiki kitu ninabadilisha, hapana! Lazima mchakato mzima wa kikodi uchukue hatamu yake ili tuweze kubadilisha sheria hiyo.

"Ndiyo maana nimesema hata lile la service levy (tozo ya huduma - inatozwa na mamlaka za serikali za mitaa) ni asilimia tatu, shilingi 100, shilingi 250 hapana! Na hili niwakumbushe wenzangu ambao tumeaminiwa kwa niaba ya watu milioni 61 wa Tanzania, sheria inapopitishwa, unapotengeneza sheria zako ndogo hakikisha hupingani na sheria ile kubwa, wafanyabiashara wameonyesha utayari wa kulipa asilimia hii tatu," alisema.

Waziri huyo pia aliwaeleza viongozi wa serikali kwamba Rais ameamua kuilea sekta binafsi, hivyo wasibadilike na kuwa kikwazo kwenye ukuaji wa sekta hiyo.

"Bila sekta binafsi hakuna uchumi wa taifa letu, ndiyo kauli ya Mheshimiwa Rais, sasa hizi tozo tunazozianzisha katikati hapa, ninaomba tuwe makini sana tusivunje sheria ambazo zinazotuongoza kuendesha halmashauri zetu. "Niwaombe sana waheshimiwa wakuu wa mikoa tulisimamie hili tuweze kulea sekta binafsi kwa maslahi mapana ya taifa letu na tupunguze manung'uniko ya ndugu zetu hawa walioshikilia uchumi wa taifa letu.

"Tunapopitisha sheria ndogo zozote kwenye halmashauri zetu, tutoke tuwape elimu wafanyabiashara wetu, wawekezaji wetu ili waelewe hizi sheria ndogo zinahusu nini na kwanini tunaleta tozo aina yoyote.

"Wakati mtu wa Osha anaeleza hapa, ni mazuri sana lakini mbona sisi hatujui tozo gani? Mwaka huu 13 zimeondolewa, Osha mbona sisi wafanyabiashara hatujui?

"Zikishaondolewa njoo utuambie ili tuzibe mianya ya watumishi wasiokuwa waaminifu kutumia mianya hiyo kutuumiza sisi wafanyabiashara. Tukifanya haya tutakuwa tumeondoka kwenye malalamiko haya," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliwaonya maofisa wa serikali wanaotumia jina la Rais kama kitisho wakati wanatekeleza majukumu yao, akiagiza tabia hiyo ikome mara moja.

## HABARI KITAIFA



Mufti Shekhe Abubakari Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mashindano ya kuhifadhi Quran ya utangulizi ya Mohamed wa sita yaliyofanyika Makao Makuu ya Bakwata. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Washtakiwa kuongezwa kesi kuvujisha mtihani la VII

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imetoa hati ya kuwakamata washtakiwa wengine ili waongezwe katika kesi ya kuvujisha Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka jana.

Ombi hilo la kutolewa kwa hati hiyo liliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Pamela Mazengo na Wakili wa Serikali, Yousuf Aboud wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa kutajwa.

Wakili Aboud alidai kuwa wana mpango wa kuongeza washtakiwa wengine katika kesi hiyo, hivyo aliiomba mahakama iwape hati ya kuwakamata watuhumiwa wanaotaka kuwaongeza.

Wakili Aboud alidai wanaendelea na upelelezi wa kesi hiyo, hivyo aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa ambapo ilipangwa Februari 2, mwaka huu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Johnson Ondieka, Patrick Chawawa, Theresia Chitanda, Elinami Sarakikya, Joyce Nkomola, Lloyd Mpande, Olomy Odongo, Docras Muro na Alcherous Malinzi.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa kuwa kati ya Oktoba 2 hadi 12 mwaka 2022, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisambaza mtihani huo kupitia mtandao wa kijamii wa Whatsapp na Telegram na kusababisha kuvuja kwa watu ambao hawakuwa na mamlaka ya kuusimamia.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hizo, Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa Malinzi alitengeneza nyaraka za uongo kuonesha kama Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba wa somo la Uraia na somo la Maadili na Maarifa ya Jamii akionesha ni halali iliyotolewa na Baraza la Taifa la Mitihani wakati akijua si kweli.

**KESI YA MRAKIBU**

Wakati huo, kesi inayomkabili aliyekuwa Mrakibu Msaidizi wa Polisi Lydya Ngua na wenzake, imekwama kuanza kusikilizwa kutokana na shahidi wa upande wa mashtaka kushindwa kufika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kutoa ushahidi.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali Slyvia Mitanto mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalira wakati kesi hiyo ilipoletwa kwa usikilizwaji.

Alidai shahidi wao ameshindwa kufika mahakamani, hivyo aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine.

Hakimu alikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Februari 6, mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mbelembe Ausi, Shabani Hamisi na Herry Chàmbo, ambao wanakabiliwa na shtaka la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu wakitumia jina la aliyekuwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Inadaiwa kuwa Januari 4, 2021, eneo la Tabata Kinyerezi jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walijipatia Sh. milioni 2.56 kutoka kwa Abdallah Said baada ya kumweleza kwamba wao ni maofisa wa polisi wametumwa na Mambosasa wamkamate kwa madai anajihusisha na utengenezaji wa vyeti feki vya kuzaliwa na vyeti vya shule wakati wakijua si kweli.

# Dada wa kazi kortini kwa madai kunyonga bosi wake

**Na Richard Makore,** MWANZA

DADA wa kazi mwenye umri wa miaka 15 (jina tunalihifadhi), amefikishwa kizimbani kwa mashtaka ya kumnyonga hadi kufa kwa kutumia mtandio aliyekuwa mwajiri wake huko Buzuruga, Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kutekeleza mauaji hayo mwishoni mwa mwaka jana kwa kumnyonga Hamida Mussa aliyekuwa Mhadhiri wa Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) jijini Mwanza.

Inadaiwa kuwa mhadhiri huyo alinyongwa hadi kufa akiwa nyumbani kwake Novemba 29, 2022 na binti huyo ambaye alikuwa mfanyakazi wake wa ndani (dada wa kazi).

Pia ilidaiwa mahakamani huko kuwa baada ya kutekeleza mauaji hayo, mshtakiwa huyo alitiwa mbaroni na maofisa wa polisi siku tatu baadaye akiwa wilayani Misungwi alikokwenda kujificha.

Mshtakiwa huyo jana alifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilemela, Fortunatus Kubaja.

Kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi ya mauaji, iliahirisha shauri hilo hadi Januari 19, mwaka huu itakapotajwa tena.

Wakati huo, hukumu ya kesi inayomkabili Mch. Diana Bundala, maarufu Mfalme Zumaridi na wenzake wanane iliyokuwa imepangwa kutolewa jana na Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Mwanza, imekwama kutokana na hakimu anayesikiliza kesi hiyo kutokuwapo.

Shauri hilo la Mfalme Zumaridi na wenzake linasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Monica Ndyekobora wa Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Mwanza.

Ushahidi wa shauri hilo ulifungwa Desemba 22, 2022 na jana ilikuwa siku ya kutolewa hukumu hiyo.

Wakati huo, Wakili wa Zumaridi, Erick Mutta amehoji mahakamani sababu za kutokukamilika kwa upelelezi wa kesi ya jinai namba 11 ya mwaka 2022 inayomkabili mteja wake.

Kutokana na malalamiko hayo ya Wakili Muta, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mwanahawa Changale alidai jalada la mshtakiwa huyo lipo kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP).

Aliahidi mahakamani huko kwamba Januari 13, mwaka huu, Ofisi ya DPP itatoa hatima na majibu sahihi kuhusu kesi hiyo.


**THE COMPANIES ACT, 2002**

**COMPANY LIMITED BY SHARES**

**SHELL TANZANIA LIMITED**

***(In Liquidation: Company Number 16839)***

**NOTICE OF FINAL GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to all the interested parties and the general public that a **GENERAL MEETING** of the Company will be held 19 January 2023 at the registered office of the liquidator, at 10: 00EAT, at which the liquidator will lay an account of the winding up of the Company and provide any explanation thereof.

| | |
|---|---|
| Liquidator (s) | **JOSEPH LYIMO** |
| Liquidator's address | **PricewaterhouseCoopers Limited, Pemba House, 369 Toure Drive Oyster Bay. P. O. Box 45. Dar es Salaam Tanzania** |

| | |
|---|---|
| Date of appointment | 1 NOVEMBER 2021 |
| By whom appointed | **MEMBERS** |

**Signed**.................................................. **Date:** 27/12/2022

**Name In Block Letters: JOSEPH LYIMO**

Joseph Cyneck Lyimo, Box 31346 Dar es Salaam, Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

217216202

# Rukhsa mikutano ya kisiasa yaibua wanasheria na wadau

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa siasa na wanasheria wametoa maoni yao kuhusu kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara na kukwamuliwa kwa mchakato wa Katiba mpya, wakieleza umuhimu wa kuwa na kamati maalum ya kupitia nyaraka zote na kuleta pendekezwa.

Aidha, wamependekeza kamati hiyo ijumuishe wataalamu kutoka nje ya nchi ambao watapitia Rasimu ya Katiba Mpya iliyoandaliwa chini ya uenyekiti wa Jaji Joseph Warioba, Katiba pendekezwa na Katiba ya sasa.

Wametaka Bunge Maalum la Katiba lisiwe na jukumu la kufumua na kuiandika upya Katiba pendekezwa bali wapitishe kwa ajili ya kupigiwa kura na wananchi.

Wamesema wananchi wanastahili kuombwa radhi kwa kunyimwa mikutano na kukiukwa Katiba kwa zaidi ya miaka sita, huku wakisisitiza kutokuwapo mikutano kumewafanya viongozi wa vijiji na mitaa kuwa miungu watu.

Wadau hao waliyasema hayo kwenye mjadala kuhusu kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa na kukwamua mchakato wa Katiba, kupitia mtandao wa 'space', uliondaliwa na kampuni ya Mwananchi juzi.

**KATIBA ILIVUNJWA**

Wakili Jebra Kambole alisema zuio la mikutano ya hadhara, lilikuwa kinyume na Ibara ya 26 (1) na Katiba ilivunjwa, ambayo inataka kila mtu kuheshimu sheria inayotoa haki ya mikutano na maoni, huku ibara ya 20 ikieleza kila mtu ana haki ya kukutana kwa amani.

"Unapozuia mikutano unakiuka ibara ya 20 (1) ya Katiba, ibara ya 21 (1), inaeleza wananchi wana wajibu wa kushiriki kufanya maamuzi yanayohusu taifa lao, kwa kuchagua na kuchaguliwa, unapozuia vyama vya siasa unakwamisha mchakato.

"Katiba na sheria hazijaweka ukomo wa kufanya siasa, kwamba mkimaliza uchaguzi shughuli zinaisha, zinaisha chama kinapokufa au mwanasiasa anapofariki, siasa sio uchaguzi ina mchakato," alisema.

Alisema vyama vina haki ya kufanya mikutano ya hadhara kujitangaza na kupata wanachama wapya na haki ya kulindwa na kupata usaidizi kutoka vyombo vya dola.

"Katazo lilisababisha wengi kupata madhara kwa vyama kuingia gharama, watu kukamatwa, kushtakiwa, kupelekwa mahakamani, ilizuia vyama kukua kwa sababu havikupata fursa kama Chama Tawala.

"Ndio maana tunasema ilikuwa kinyume cha sheria, katazo lilikuwa kinyume cha sheria na Katiba, wanasiasa na wananchi wana haki ya kuombwa msamaha, pamoja na ruhusa kutolewa sio jambo la kubeza," alisema.

Kambole alisema ni muhimu kuchakata sheria zilizoko ili chama kinapozuiwa kufanya mikutano kielezwe sababu za wazi na zijadiliwe kuliko polisi kutumia nguvu.

Kuhusu Katiba Mpya, alisema ni muhimu kuundwa kamati ya wataalamu wa Katiba na ijumuishe watu kutoka ndani na nje ya nchi ili wafanye uchambuzi wa rasimu ya Katiba ya Jaji Joseph Warioba Pendekezwa na Katiba ya sasa ya mwaka 1977.

"Tunataka Katiba inayojilinda yenyewe tunaita Nungungu, aihitaji mwanasiasa wa kuilinda, inafanya uwajibikaji yenyewe, mnapata kiongozi huru, inapata jaji huru kwa namna ilivyotengenezwa, kujipendekeza ni mtu mwenyewe na sio mrengo wa Katiba," alifafanua.

Naye John Heche, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, alisema taswira aliyonayo ni kila chama kinachojiandaa kushinda na kuongoza nchi, ndivyo ipasavyo kupewa fursa ya kujiimarisha na kujitangaza.

"Ukisoma sheria hii namba 5 ya vyama vya siasa kifungu cha 11, imeruhusu taarifa itolewe saa 48, polisi itatoa ruhusa ya mikutano ya hadhara, kama wanaona viwanja vitaingiliana wanaweza kutoa ushauri eneo la sokoni litumike," alisema Heche.

**MIUNGU WATU**

Alisema katazo la mikutano ya hadhara, liliathiri zaidi maeneo ya vijijini kwa kuwa wenyeviti wa vijiji baadhi yao walijimilikisha mamlaka kibinafsi na kutowajibika, huku viongozi wengine wakichukia ukosoaji dhidi yao.

**CHAWA WA RAIS**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Faraja Kristomus, alisema "Tunapotoa sifa kwa Rais Samia tukumbuke anaungwa mkono na viongozi wenzie wa ngazi za juu ndani ya CCM, pia mazingira ya kisiasa na shinikizo lililokuwapo kwa wakati huu wa sasa yanalazimu siasa za ushindani kuruhusiwa kwa sababu ni mambo muhimu na nyakati zimebadilika.

"Ili aweze kufurahia mazingira ya kuitawala lazima watu wamkosoe kama yeye mwenyewe alivyotahadharisha kuwa wasimtukane bali wamkosoe.

"Sasa changamoto inakuja kutoa tafsiri sahihi ya kukosoa na kutukana, wakati mwingine Rais hawezi kukosolewa tu, lakini wafuasi wake ambao kwenye msemo wetu wa mtaani wanaitwa 'chawa' wakadhani anatukamwa hii ndio shida inaweza kuja hapo baadaye."

Kristomus alisema waliopo ndani ya CCM na watendaji kwa ujumla wanapaswa kukubali hali halisi kwamba wananchi watapata fursa ya kusikiliza sera tofauti, kwa sababu ni wakati mwafaka kwa vyama vya upinzani, miaka miwili kabla ya uchaguzi mkuu 2025 na uchaguzi wa serikali za mitaa 2024.

Alisema ni nafasi nzuri kwao kuendelea kuuza sera zao na kupata idadi mpya ya wafuasi, kuwatafuta wanachama wapya na kuwarejesha walioondoka.

Kuhusu Katiba Mpya, Dk. Faraja alisema ni muhimu kuwapo kabla ya 2025, ili kuvuna matunda ya uhuru yaliyojengwa na Rais Samia, kwa vyama vya siasa kujieleza kwa wananchi, kuwezesha mazingira huru ya uchaguzi na usimamizi.

Alisema endapo mchakato wa Katiba Mpya utafanyika baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, matunda ya maridhiano na ruhusa ya mikutano ya hadhara hayataonekana sasa na kwamba ni muhimu mchakato ukamilike mwakani, ili Tume ya Uchaguzi iwe na mamlaka ya kuandaa uchaguzi kwa Katiba Mpya.

"Tunaamini tutakuwa na uhuru mpana wa kufanya uchaguzi wa 2025, tutakuwa na wawakilishi tutakaowapata kwa kupitia Katiba Mpya na hivyo tutatoa nafasi kwa wananchi.

"Matunda ya mchakato ambao Rais Samia ameutangaza sasa, tukiruhusu upatikane baada ya 2025 tutaendelea kukipa nafasi CCM kupata ushindi zaidi na demokrasia tunayoilillia hatutapata matunda," alifafanua.

Robert Maura, alisema Rais kuruhusu mikutano ya hadhara kisigeuke kuwa pongezi, kwa sababu tayari kauli ya kusitisha mikutano iikuwa kinyume cha Katiba ya nchi.

"Tunachoweza kusema ni kaiheshimisha Katiba, sio kupongezwa. Tunahitaji tuwe na Katiba Mpya kwanza kabla ya tume huru," alisema Robert.

**CCM YAWAKARIBISHA**

Prof. Kitila Mkumbo, alisema yeye akiwa mmoja kati ya wabunge kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamejiandaa vyema majimboni kupambana na wapinzani, kwa kuwa tayari wameanza kuwaambia wajiandae.

"Mimi nikiwa kama mbunge wa CCM pamoja na wabunge wenzangu, tunasema kwamba tumejiandaa ipasavyo, tunawakaribisha majimboni tufanye siasa, CCM hatuogopi mikutano wala kukosolewa waje tubishane kwa hoja, waseme ukweli na sio uongo," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan

**ACT-WAZALENDO**

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema baada ya Rais Samia kuingia madarakani walikuwa wakifuatilia mtiririko wa uongozi wake na chama kikaridhika.

"Ahadi yake, maono yake ya kufungua nchi ya Tanzania, yanapaswa kuungwa mkono, tukafanya kama vile Waingereza wanasema 'benefit of doubt' yeye mwenyewe katuthibitishia anayonia ya dhati kama matamshi yake," alisema Ado.

Alisema kupitia hatua nne, chama hicho kilianza kwa kuandika barua kwa kumuunga mkono kuhusu siasa, majadiliano ya vyama, kushiriki kwenye kituo cha demokrasia na pia katika kikosi kazi kilichoundwa na Rais, kwa kutoa maoni.

Baada ya hatua hizo zote, wadau wa demokrasia nchini walianza kutoa maoni, hasa baada ya tamko la kuruhusu mikutano, akisema ni mwanzo wa siasa za kistaarabu na maelewano.

**WATAKA KALENDA**

"Tunaamini Rais atatembea kwenye mstari kama alivyotuahidi, sasa iwapo kalenda siku gani tutaenda kurekebisha sheria ya vyama vya siasa, ya dharura ya Jeshi la Polisi na jinsi gani ratiba ya katiba mpya," alisema Ado.

Alisema ni vyema pia, wadau wa siasa nao wakabaini muda uliosalia kujiandaa kisiasa hasa mwaka ujao umekaribia na joto la uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Tuna mwaka mmoja tu wa kuelekea 2024 mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa. Suala lingine ambalo rais ametupa na tumaini kuna kukosekana kufungamana, baina anachokisema rais na kilichotokea nchini," alisema Ado.

Alisema unahitajika ufuatiliaji wa utekelezaji na mfungamano baina ya watendaji, akisema baadhi yao wanadhani mbinu rahisi zinaweza kurahisisha chaguzi, jambo ambalo si sahihi, kwa kuwa uwapo wa ushirikiano kati wa wanasiasa na watendaji kwenye siasa ni muhimu.

"Mienendo ya Jeshi la Polisi bado haiendani na hiki, hata tulipofanya mikutano ya ndani, utakuta mikutano bado viongozi wetu wanapata 'summon'," alisema Ado.

Kadhalika, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya siasa nchini, Juma Khatibu, alisema zuio la miaka takribani sita kufanya mikutano ya hadhara kisiasa, kulirudisha nyuma vyama vya kisiasa na kwamba rais apongezwe kwa kuondoa zuio.

"Rais amewaweka Watanzania katika kitu kimoja, alizungumza kwa ukweli na uwazi kabisa, sisi wanasiasa tushirikiane na kauli ya rais, hata tukikosoa tukosoe kwa staha, niseme kitu kimoja, baadhi ya marais wa Afrika hupewa tuzo mbalimbali kwa kusimamia vyema nchi zao, nafkiri rais anastahili," alisema Juma.



Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Zuwena Omari (kushoto), akimkabidhi cheti cha Kampuni ya GoMama Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Mariam Ulega katika hafla iliyofanyika jana mjini Kibaha.
PICHA: JULIETH MKIRERI

# Kamati Bunge kuanza na ukaguzi wa CAG

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI za Kudumu za Bunge zinatarajiwa kuanza vikao Jumatatu jijini Dodoma ambavyo vitafanyika hadi Januari 29, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Bunge, kamati hizo zinakutana kabla ya mkutano wa 10 wa Bunge utakaoanza Januari 31, mwaka huu.

Aidha, kamati hizo pia zitachambua taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuhusu ukaguzi maalum na ukaguzi wa ufanisi utakaofanywa na kamati mbili za kudumu za kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi zitaanza vikao Januari 9, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, shughuli zitakazofanyika ni kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa za mwaka za shughuli za kamati zilizowasilishwa bungeni Februari, mwaka jana.

Kamati hizo pia zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali kuhusu shughuli za umma nchini ili kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya sekta zinazohusika.

Kazi nyingine ni kupokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma, ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu, sheria na miongozo mujarabu ya biashara.

Pia kamati hizo zinatarajia kupokea na kujadili taarifa kutoka kwenye wizara na taasisi mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa vyanzo vya mapato na utekelezaji wa bajeti.

Aidha, kamati ya sheria ndogo itachambua sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa mkutano wa tisa, pamoja na kupokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria hizo iliyowasilishwa katika mkutano wa tano, sita na saba wa Bunge.

## Miili watoto wawili wa familia moja yakutwa ikielea kisimani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WATOTO wawili wa familia moja wamekufa maji baada ya kuzama kwenye kisima wakati wakicheza eneo la Nyatorotoro, mkoani Geita.

Umri wa watoto hao umetajwa kuwa ni miaka mitatu na mwingine mwaka mmoja na nusu, hata hivyo, majina yao hayajajulikana na miili yao imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Mkoa wa Geita kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapo, Edward Lukuba, alisema tukio hilo lilitokea Januari 5, mwaka huu, majira ya saa 11 jioni.

Lukuba alisema walipata taarifa hizo na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walienda hadi eneo la tukio na kukuta miili ya watoto hao ikielea juu ya maji kwenye kisima.

Alisema askari hao waliitoa miili na kuipeleka Hospitali ya Mkoa wa Geita kwa uchunguzi zaidi.

Aidha, alisema chanzo cha vifo hivyo ni uzembe wa wazazi na kulaani kitendo hicho cha kushindwa kuangalia watoto wao kwa kuwaacha wanacheza karibu na kisima.

Kaimu Kamanda, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Geita kuweka uzio kwenye visima vya maji pamoja na kuvifunika ili kuokoa maisha ya watoto.

# Kimbisa akoleza moto pongezi kwa Rais Samia

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Adam Kimbisa, amesema kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan, kuruhusu mikutano ya kisiasa ni sehemu ya mwendelezo wa jitihada za kuhakikisha mazingira ya ufanyaji siasa nchini yanaboreka.

Jumanne wiki hii, Rais Samia aliondoa rasmi katazo la kufanya mikutano ya hadhara ya kisiasa hatua iliyopongezwa na na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Jijini Dar es Salaam, Kimbisa ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, alisema hatua hiyo pia itasaidia kuimarisha hali ya demokrasia, uhuru wa vyombo vya habari, mahusiano ya vyama vya siasa na uhuru wa kujieleza.

Alisema alichokifanya Rais Samia ametimiza uwapo wa siasa safi na uongozi bora na kwamba uamuzi wake siyo tu umekuwa nguzo muhimu ya kuchochea kasi ya maridhiano ya kisiasa nchini bali imechangia kuondoa mkwamo wa kisiasa uliokuwapo kwa miaka sita.

"Hatua aliyochukua Rais Samia pia inathibitisha ukomavu alionao, weledi, uthubutu na nia yake nzuri kwa Watanzania kwa ujumla wetu. Anapaswa kupongezwa na kila mtanzania mpenda maendeleo bila kujali vyama vyetu, dini wala rangi zetu," alisema Kimbisa.

Aliongeza kuwa Rais Samia sasa kawaruhusu kuongea na kuwasiliana na wananchi na kwamba katika hatua hiyo kuna vyama vitakwenda kutafuta wanachama zaidi au kuwaboresha huko waliko.

Aidha, alisema CCM Mkoa wa Dodoma inaamini kwamba kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara kutaimarisha nguvu ya kisiasa, kutapanua wigo kwa wanachama wengi zaidi kutoa mawazo yao juu ya masuala mbalimbali yanayohusu taifa. Alisema hatua hiyo itafungua fursa kwa wanachama wa ngazi zote kunadi na kutangaza hadharani mazuri yote yanayofanywa na serikali na kwamba hiyo ni hatua kubwa ya kuelekea kupata maendeleo endelevu.

"Ni matumaini yetu kwamba fursa hii iliyotolewa na mkuu wa nchi, itatumika vizuri na itakuwa chachu ya kuzalisha mawazo bora kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu, tuwaombe Watanzania wote kuendelea kumuunga mkono Rais Samia, tumuombee busara na maono ili aendelee kulifanyia taifa letu mambo makubwa zaidi," alisema Kimbisa.

Hata hivyo alisema kwa kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake, Rais Samia amefanya mambo makubwa hususani kwenye demokrasia, uhusiano kimataifa, miundombinu, afya, elimu, nishati, ulinzi na usalama na uhuru wa habari.

Aliahidi kuwa CCM Dodoma watafanya siasa za kistaarabu, zisizo na lugha za maudhi, vurugu na maandamano yasiyokuwa ya lazima ili kuonyesha ukomavu wa kisiasa kwa maslahi mapana ya taifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio ya kujiua, kuua yanaweza kudhibitiwa

**MATUKIO** ya watu kujiua au kuua wenzao yanaweza kudhibitiwa kama ushauri wa madaktari na wanasaikolojia utafuatwa.

Mengi ya matukio hayo yanaelezwa kusababishwa na hasira na mihemko ambayo kama itadhibitiwa mapema itapunguza madhara.

Elimu kwa jamii ni jambo muhimu kwa sababu itawafanya watu kuelewa vitu vya kuepuka wanapoona viashiria vyovyote vya vitendo vya mauaji.

Imeshauriwa pia watu wanapohisi hali isiyo ya kawaida kuondoka eneo ama mazingira yanayochochea kutenda mambo mabaya na njia hiyo imetajwa kuwa dawa inayoweza kudhibiti ama kupunguza matukio ya watu kujiua au kuua.

Daktari Bingwa wa Binadamu, Idara ya Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Raymond Mgeni, anaeleza kuwa jamii inapaswa kudhibiti msukumo wa hasira unaochochewa na sababu yoyote, ikiwamo kuudhiwa ama kusingiziwa jambo lolote kwa sababu ni kati ya visababishi vya ongezeko la matukio ya mauaji nchini na ukosefu wa kudhibiti hali hiyo.

Takwimu zilizotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka juzi kuhusu haki za binadamu, zinaonesha kuwa watu wanne kati ya 10 waliojiua mwaka jana (2021), walikuwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Ili kudhibiti matukio ya watu kujiua au kuua jamii inapaswa ijenge mazoea na utaratibu wa kujifunza na kuwafundisha watoto, kutoruhusu kuchukua hatua wapatwapo na msukumo huo na kuondoka eneo ama mazingira yanayosababishia hasira.

Daktari anafafanua kuwa matukio yanayoongezeka ya watu kujiua hutokana na kuchochewa na misukumo isiyodhibitiwa kutokana na hasira, ikiwamo mazingira yanayowazunguka na kusababisha mtu kuamua jambo bila kutarajia na kufahamu athari zake baadaye.

"Kuna wakati mwingine unaongea na mtu anakuudhi, kuna wengine hawana udhibiti, wengine wanaoudhiwa wanapoambiwa jambo ambalo hawajalitenda wanajikuta wakipatwa na hasira, akipandwa na hasira anaweza kuchukua kitu ajichome au anywe sumu."

Hali hiyo pia inaweza kuchangia kisasi na matukio mengi. Watu walikuwa kwenye mazungumzo wakapishana kauli mmoja ananyanyua jiwe au chupa na kumrushia mwenzake. "Idhibiti hali hiyo na iwe ni utaratibu kwenye maisha yetu kila siku."

Ripoti ya LHRC kuhusu haki za binadamu kwa mwaka 2021/22, inazungumzia haki ya kuishi inavyokiukwa kutokana na matukio kadhaa hasa ongezeko la mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi.


Ripoti hiyo inasema wanawake ndiyo waathiriwa wakuu wa matukio ya ukatili wa kijinsia, wanauawa na wapenzi wao kwa sababu ya wivu wa mapenzi, ingawa takwimu zinabainisha pia wanaume ambao wanaongoza kwa kuchukua maamuzi magumu ya kujiua.

Kadhalika, takwimu za Shirika la Afya Dunani (WHO), zinaonesha kwamba Watanzania milioni saba, wana tatizo la afya ya akili wengi wao wakiishi Dar es Salaam.

Pia kuna mtu mmoja hufariki dunia katika kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Aidha, takwimu za LHRC kuhusu haki za binadamu mwaka 2021, inabainisha kwamba watu wanne kati ya 10 waliojiua mwaka jana (2021) walikuwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchunguzi ufanywe, kulikoni matusi kwenye mtihani, kidato 2 kuporomoka

**MOJA** kati ya mambo yaliyotawala kwenye matokeo ya mitihani ya kidato cha pili na darasa la saba ni kushuka viwango ya ufaulu, kuwapo udanganyifu pamoja na matusi.

Kaimu Katibu Mkuu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa, Athumani Amasi, anasema kwamba wanafunzi 279 wamefutiwa matokeo, kati yao 82 ni wa darasa la saba na 213 wa kidato cha pili.

Akasema hao walifutiwa, baada ya kubainika kuwa wamefanya udanganyifu na 14 wa kidato cha pili waliandika matusi.

Pia, kwenye mtihani wa kidato cha pili, kunatajwa ufaulu ulishuka na kuwa asilimia 82.6.7 dhidi ya asilimia 92.3.2 kwa msimu uliopita.

"Natoa wito kwa wazazi, walezi kuacha tabia ya kuwadanganya wanafunzi ambao ni watoto wao kwa mbinu tofauti ili wafaulu, waache wafanye mitihani kwa uwezo wao, wakiandaliwa vizuri watafaulu," alisema Amasi.

Nawapongeza wanafunzi wote wa kidato cha pili na darasa la nne waliofaulu. Hata ambao hawakufanikiwa, wasikate tamaa, kwani inawezekana hawakuwa kwenye hali nzuri wakati wa mitihani.

Inawezekana kabisa siku hiyo walikutana na changamoto mbalimbali. Huwezi kujua wanafunzi wanapitia mengi sana, inawezekana siku hiyo akatoka nyumbani kukiwa na ugomvi wa wazazi wake, au siku ameamka akiwa anaumwa, hata kufiwa.

Wanaweza kurudia tena Mungu akawasaidia.

Kuna wale ambao wanadanganya, tena kwa kusaidiwa na wazazi na walezi wao kama alivyosema Amasi.

Hii inatokana na dunia ya sasa kuhitaji zaidi vyeti kuliko uwezo halisi wa mtu. Ndiyo maana wazazi wanatumia sana kuwapa kile wanachokuona kama ni majibu ili wafaulu bila hata kujali kichwani mwa watoto wao kuna nini.

Hii ndiyo inatuzalishia wasomi 'feki' ambao waajiri wengi wanadai hawaajiriki, kwa sababu wamefuzu kwenye makaratasi tu kwa uongo. Wale wenye uwezo wanaachwa. Halafu wazazi kama hawa wanawapa matokeo watoto wao, wakifaulu wanafanya bonge la sherehe.

Hawa wazazi hawana tofauti na timu inayonunua mechi, halafu ikipata ubingwa inafanya sherehe ya kuwa bingwa.

Mimi nadhani imefika wakati wataalamu wetu na wasomi, kuanza uchunguzi kujua ni kwa nini ufaulu msimu huu umepungua, pia kwanini miaka ya hivi karibuni kumekuwa na udanganyifu kwenye mitihani kiasi kwamba inafikia wakati watu wanabadilisha hata namba za watahiniwa na hata wale wanaoandika matusi.

Naweza kuonekana wa ajabu kidogo kwa sababu ya utamaduni wetu. Huwa si watu wa kufanya uchunguzi, lakini hili kwa wenzetu wangelifanya haraka sana, halafu wangekuja na majibu.

Hayo majibu huwa yanazisaidia serikali kujua nini cha kufanya. Nini cha kupunguza na nini cha kuongeza.

Tuna wasomi wengi nchini ambao wamekaa tu, huu sasa ni wakati wa kuwaingiza kwenye mtihani wa kufanya uchunguzi.

Ni kuwachukua hao wanafunzi, kukaa nao kirafiki tu, na kuwauliza ni nani anawapa mitihani na walielezwa nini, na hata wanaotukana wanafanya hivyo kwa sababu gani, na kipi huwa kinawasibu.

Hapa tunaweza kupata kitu tusichokijua tofauti na tunavyofikiria. Hadi sasa hatujajua ni kwa nini miaka kadhaa iliyopita kuna mwanafunzi alichora zombi kwenye mtihani.

Vitu kama hivi sisi tunaviona kama mzaha, lakini wenzetu huvichukulia kwa umakini na kupata somo ambalo linawafanya kurekebisha hali fulani ya kuokoa wanafunzi na kuwafanya warudi kwenye mstari wao na wazazi wao wanaotaka watoto wao wafaulu bila ya kuwa na uwezo kichwani.

HABARI KITAIFA

# TEF yajipa matumaini mabadiliko Sheria ya Habari ya Mwaka 2016

**Na Mwandishi Wetu**

DEODATUS Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), amesema mwaka 2023 serikali itaonyesha kwa vitendo kile ilichokiahidi tangu mchakato wa mabadiliko ya vipengele vya sheria ya habari uanze.

Amesema isingekuwa rahisi kuwa na matumaini hayo iwapo serikali ingeamua kuyapa mgongo malalamiko ya wadau wa habari nchini kuhusu vipengele vinavyozuia ukuaji wa sekta ya habari nchini kwenye sheria hiyo.

Akizungumza na mwandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Balile alisema ushirikiano wa serikali hususani Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari chini ya Waziri wake, Nape Nnauye, umeifanya tasnia ya habari kuwa na matumaini tele ndani ya mwaka huu.

"Mheshimiwa Nape atakumbukwa katika hili, lakini nguvu kubwa kaipata kutokana na Mheshimiwa Rais kwa kuwa 'positive' (chanya) na jambo hili. Ni matarajio yetu kwamba mwaka huu wa 2023 utaleta mageuzi katika tasnia ya habari.

"Sisi huku kwenye mikutano ya wadau tumeshamaliza, kikao cha mwisho tulifanya Novemba 21, 2022 na baadaye tukaongeza na Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari 2022 lililofanyika Desemba 18, 2022.

"Hivyo kilichobaki ni Muswada wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 kuwasilishwa bungeni baadaye mwezi huu," alisema Balile. Alisema wadau wa habari wanaamini kuwa mawazo yao waliyokubaliana na serikali katika maeneo yote, ndiyo yatakayokuwamo kwenye muswaada huo.

Mwenyekiti huyo wa TEF alisema matarajio ya wadau wa habari ni kuona muswada huo wa mabadiliko ya sheria ukisomwa bungeni Januari mwaka huu.

"Kwanza kabisa, utapitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kisha utajadiliwa na Kamati ya Makatibu Wakuu na baada ya hapo utajadiliwa na Kamati ya Baraza la Mawaziri.

"Ukitoka hapo utajadiliwa na Baraza la Mawaziri, tunarajia itakuwa kati ya Januari 13 na 14, matazamio yetu ni kwamba utasomwa bungeni kwa mara ya kwanza Januari 31, mwaka huu kisha tutakutana na wadau kuzungumza na wabunge baadaye utasomwa kwa mara ya pili na utajadiliwa," alisema Balile.

Kiongozi huyo wa TEF alisema kwamba kupitia kauli ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape, aliyotoa siku ya Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari 2022, muswada huo utawasilishwa bungeni katika Bunge linalokuja.

"Kwa kauli ile ya Mheshimiwa Waziri tunaimani kuwa muswaada huo utaingia Bunge hili la Januari na maisha mengine yaendelee," alisema Balile. Akizungumzia kuhusu mabadiliko ya Sera na Sheria nyingine katika sekta ya habari, Balile alisema wataziona mbele ya safari.

Desemba 18, mwaka jana, akizungumza wakati wa Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari 2022, Waziri Nape alisema serikali ina mpango wa kurekebisha sekta ya habari kupitia mfumo wa kisheria, ikiwa ni pamoja na kuunganisha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010.

Waziri Nape alisema hatua hiyo inatarajiwa kuleta uratibu madhubuti wa sekta hiyo na umoja kati ya wahusika katika magazeti, mitandao ya elektroniki na kijamii kwa kuwa zote ziko chini yake.



Mkuu wa Idara ya Huduma Mbadala Kupitia Mifumo ya Kidigitali, Benki ya Exim, Silas Matoi (wa pili kulia), pamoja Meneja wa Tawi la Exim Tower, Vishal Ratansinh (kulia) na Ofisa Idara ya Huduma Mbadala Kupitia Mifumo ya Kidigitali, Gregory Malembeka (kushoto), wakikabidhi zawadi ya simu janja aina ya Iphone 14 Pro kwa Balubhai Patel mkazi wa Dar es Salaam baada ya kuibuka mshindi wa droo ya pili ya mwezi katika kampeni ya Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yajizatiti uwekezaji kilimo cha mpunga

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI ya Zanzibar imeanza uwekezaji katika kilimo cha mpunga kwa kutenga Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Uwekezaji huo utawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na tija kwa kutumia mbegu za teknolojia za kisasa ambazo zina ukinzani wa magonjwa ya zao hilo.

Katika kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa, tayari Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia Kilimo, Biashara na Utalii, imeamua kwenda kujifunza kilimo hicho katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Dakawa, kilichoko Mvomero mkoani Morogoro ambacho kinashughulika na utafiti wa zao hilo.

Akizungumza akiwa TARI Dakawa, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Zanzibar, Shamatha Khamis, alisema pamoja na kufanya kilimo hicho, hivi sasa wameongeza miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji cha mpunga ili kuongeza uzalishaji kwa ajili ya kukuza uchumi wa buluu.

Waziri huyo alisema tayari wameshajenga skimu za umwagiliaji sita na sasa wanatarajia kuanza uzalishaji, hivyo wameamua kutembelea kituo hicho ili kujifunza mbinu za kisasa za uendeshaji wa kilimo cha mpunga.

"Tumeona tusianze kufanya kilimo hiki cha umwagiliaji katika zao la mpunga moja kwa moja bila kuja kujifunza mbinu mbalimbali. Tunashukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kwa kutukubalia ombi letu kuja TARI Dakawa," alisema.

Alisema kupitia ziara hiyo, wamejifunza aina mbalimbali za mbegu ya mpunga ambazo zingine wanazo na zingine hawana lakini zinafanya vizuri katika uzalishaji, hivyo watatumia nafasi hiyo ya mafunzo kujikosoa au kujiweka sawa ili kufikia malengo ya uzalishaji.

Hata hivyo, waziri huyo alisema bado kuna changamoto kuhusu pembejeo za ruzuku ambazo kwa Zanzibar hakuna lakini kutokana na ushirikiano kati ya serikali ya Muungano, wanaamini watafanya mazungumzo kuhakikisha mgawo huo unawafikia wakulima wa Zanzibar. Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema wako tayari kwa ajili ya kutoa wataalamu kwenda kutoa elimu ya kilimo hicho visiwani Zanzibar kwa kuwa imeshagundua teknolojia za kutosha za mbegu za kisasa ambazo zinahimili ukinzani na magonjwa pamoja maeneo mbalimbali yakiwamo yenye chumvi na magadi.

Dk. Mkamilo alisema TARI ina mbegu bora 54 za mazao mbalimbali ambazo zinafanya vizuri na kuongeza uzalishaji na kupambana na wadudu waharibifu pamoja na mbinu za kilimo bora cha mazao likiwamo la mpunga.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Mbaroni kwa tuhuma za kumuua mkewe, kumfukia shimo la choo

**Na Lilian Lugakingira,**
MISSENYI

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Simon Samson (30), mkazi wa Kitongoji cha Mubembe, Kijiji cha Kakindo wilayani Missenyi kwa tuhuma za kumuua mke wake, Melines Jonathan (34) na kumfukia kwenye shimo la choo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa kijiji hicho, Sprian Bagaiga, Melines alipotea tangu Desemba 20, mwaka jana na kwamba alipewa taarifa hizo na wananchi Desemba 28, mwaka jana.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa baada ya kupata taarifa alifanya jitihada za kumtafuta na juzi mwili wake ulikutwa umefukiwa kwa udongo kwenye shimo la choo cha nyumba alipokuwa akiishi, huku tayari ukiwa umeharibika.

Alisema kuwa wakati wakimtafuta mama huyo, walipofika karibu na choo kulikuwa na harufu kali na alipochungulia aliona mkono.

"Nikachungulia kwenye choo hicho, nikaona mkono wa binadamu na eneo hilo kulikuwa na harufu kali, tulitoa taarifa polisi na walipofika walikuta mtuhumiwa tumekwishamkamata," alisema.

Mwenyekiti alisema kuwa baada ya polisi kufika choo kilibomolewa na udongo uliokuwa umetumika kumfukia ukaondolewa, ndipo ikathibitika kuwa ni mwili wa binadamu.

Alisema kuwa kutokana na mwili huo kuharibika, waliona matiti na ndipo wakabaini kuwa ulikuwa mwili wa mwanamke.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kabla ya mauaji hayo, wawili hao walikuwa na ugomvi wa mara kwa mara unaohusishwa na wivu wa mapenzi.

Alisema kuwa mara ya kwanza mtuhumiwa aliwahi kumkaba shingo mwanamke huyo akitaka kumuua, lakini wananchi wakamwokoa na mara ya pili akachukua panga akataka kumkata, majirani pia wakamwokoa.

Alisema kutokana na ugomvi wa mara mkewe alimfukuza mwanamume huyo kwenye nyumba aliyoijenga mama huyo na akarudi nyumbani kwao na baadaye akawa anarejea kwa mkewe.

Mmoja wa majirani walioshuhudia tukio hilo, Remigius Fidelis alisema kuwa kabla ya mwili wa mama huyo kugundulika kuwa upo kwenye shimo la choo, harufu ilianza kusambaa kwenye eneo hilo, hali iliyowafanya wawe na hofu.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na wanamshikilia mtu mmoja kwa tuhuma za kuhusika na mauaji hayo.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mhandisi Tamimu Katakweb (kushoto), kuhusu kukamilika kwa mitambo ya kusukuma maji katika eneo la Kiegea A na B Manispaa ya Morogoro, (katikati) ni Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood. **PICHA: ASHTON BALAIGWA, MOROGORO**

# Waziri asema mbunge anamnyima usingizi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood ni miongoni mwa wabunge ambao wamekuwa wakimnyima usingizi kutokana na kuhoji mara kwa mara kuhusu kero ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

Aweso amesema Bunge lina wabunge wengi lakini Abood ni wa aina yake kutokana na kufuatilia utatuzi wa kero ya maji kwa wakazi wake wa eneo la Mguluwandege, Mkundi Kihonda, Kilakala na Bigwa, Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza wakati akikagua mradi wa maji wa Mguluwandege jana, Waziri Aweso alisema tatizo la maji kwenye maeneo hayo sasa litabaki kuwa historia kutokana na serikali kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji kwa Manispaa ya Morogoro.

"Tumeshuhudia kukamilika kwa ujenzi wa tangi kubwa la lita milioni mbili, tumekwenda Kiegea, tumeona tangi lingine la lita milioni moja litahudumia Kiegea A na B, Kilimanjaro na eneo la Reli yetu ya Mwendokasi.

"Tangi la Mguluwandege linakwenda kutatua tatizo la maji kwa wakazi wa Mkundi, Kihonda mpaka Lukobe. Hii yote ni jitihada za Mbunge wenu Abood kwa kufuatilia ili tatizo hili la maji liweze kuisha na sasa linaisha kabisa, itabaki kuwa historia," alisema.

Waziri huyo alisema hakuna sababu ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro kukosa maji kwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Morogoro (MORUWASA) imeshapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

"Mkoa wa Morogoro kulalamika masuala ya maji ni aibu kwa Wizara ya Maji, hivyo nikuhakikishie mbunge miradi hii yote tutahakikisha inakamilika kwa wakati ili wana Morogoro waweze kupata majisafi na salama kwani maji hayana mjadala," alisema Waziri Aweso.

Mbunge wa Morogoro Mjini, Abood, alisema anafurahi kuona kata zote zilizokuwa na kero ya maji zinapata maji na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kukamilisha miradi hiyo.

"Ni kweli kabisa kila hoja yangu bungeni ni maji na hata wewe waziri tukikutana kwenye korido salamu yangu ni maji ila ninakuomba ule mradi wetu mkubwa wa maji wa Sh. bilioni 185 sasa uanze utekelezaji wake baada ya kukamilika miradi hii midogo," alisema Abood.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Tamimu Katakweba, alisema wameshafanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ukosefu wa huduma za majisafi baada ya kukamilika kwa miradi midogo ya maji na kinachosubiriwa ni kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa utakaohusisha Bwawa la Mindu ambao utamaliza kero hiyo kabisa na kuwa na maji ya ziada.

## Chanika na Buyuni kupata uhakika wa maji Februari

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB) wanatekeleza mradi wa maji wa Sh. bilioni 22 utakaonufaisha wananchi 210,000 katika wilaya tatu za Temeke, Ilala na Kigamboni.

Utekelezaji wa mradi huo wa uboreshaji huduma ya majisafi maeneo ya pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam umeendelea kushika kasi na umeshafikia asilimia 61.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo jana, Msimamizi wake, Stephen Urio alisema mradi umegawanyika katika awamu mbili za utekelezaji na chanzo cha maji cha mradi huu ni mitambo ya Maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na visima virefu vya Nzasa na Kimbiji.

Aliongeza kuwa awamu ya kwanza imehusisha ulazaji wa mabomba ya maji ya ukubwa tofauti kwenye mitaa 13 kwa umbali wa kilomita 137.5 pamoja na kuunganisha wateja zaidi 2,000.

"Katika awamu hii tumeshalaza mabomba ya umbali wa kilomita 120 na kazi inaendelea, uunganishaji wa wateja utafanyika kwa awamu hasa kwenye maeneo ambayo tayari ulazaji wa mabomba umekamilika katika kata za Chamazi na Buyuni," alisema.

Katika awamu ya pili, Urio alisema mradi umehusisha ujenzi wa tangi la maji kwenye eneo la Somelo - Chanika lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni mbili na ulazaji wa mabomba umbali wa Km 69.2 na ufungaji wa pampu moja yenye uwezo wa kusukuma maji lita milioni 60 kwa saa na kwamba ujenzi wa tangi la maji umefikia hatua ya kusuka nondo za ukuta na umwagaji wa zege la kwanza la ukuta.

"Mpaka sasa mabomba yaliyolazwa kwa awamu ya pili ni kilomita 52 kati ya kilomita 69.2," alisema.

Alisema mradi unatekelezwa katika wilaya tatu ambazo ni Temeke, Ilala na Kigamboni ndani ya kata tisa na mitaa 19 ambayo ni Ferry, Tungi, Magogoni, Upendo, Mwanamtoti, Butiama, Mlanzini, Dovya, Kisewe, Magengeni, Mwembe Bamia, Mgeule, Mgeule Juu, Nzasa, Somelo, Kifurukwe, Uvumba, Kichangani na Yangeyange.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nzasa, Hashim Yasini, aliomba DAWASA kusimamia kwa karibu zaidi utekelezaji wa mradi huo ili wananchi wanufaike na huduma ya maji kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo sasa wanapata maji kupitia visima vya asili.

"Tunaona kasi yao ni kubwa, maana tunawatembelea makandarasi mara kwa mara na tumejitahidi kushirikiana nao wanapopata changamoto ya maeneo ya kupitisha bomba, tunatoa ushirikiano mkubwa ili mradi usikwame," alisema.

# Wananchi walia tembo kuyavamia makazi yao

**Na Christina Haule,** MVOMERO

WAKAZI wa Kijiji cha Lubungo Kata ya Mlali wilayani Mvomero mkoani Morogoro wamesema licha ya serikali kuwapelekea maji kupitia mradi wenye thamani ya Sh. milioni 400, kuna haja hatua stahiki kuchukuliwa kudhibiti tembo wanaozagaa kwenye eneo lao na kuharibu mazao, pia kuhatarisha uhai wao.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Kasoko Tokoyeti, alisema walikuwa wanakabiliwa na shida ya maji na kuyafuata maeneo ya mbali kwa baiskeli na wakati mwingine hulazimika kunywa maji ya madimbwi hasa nyakati za mvua kutokana kushindwa kwenda kuchota maji kwenye chanzo kutokana na kikwazo cha tembo.

"Tunafurahi kupata maji, kweli maji ilikuwa shida yetu na tembo waliozidi yatatusaidiaje? Mtatuonea huruma, hatuwezi hata kulima, mimi leo usiku nimepambana nao tembo nyumbani kwangu, wamekula maembe, wamemaliza mazao yetu yote," alisema.

Tokoyeti alisema wakazi wa kata hiyo hulima mazao ya mahindi, mihogo, miwa na migomba na hawana shida ya chakula, muda wote lakini miaka mitatu mfululizo hawajapata mavuno ya kutosha kutokana na ndovu hao kuharibu mazao yao.

Alisema adha ya ndovu imekuwa ikiwalazimu wazazi kuwasindikiza watoto wao shuleni asubuhi kwa kuhofia kukutana na makundi ya wanyamapori hao na kupata madhara.

Mbunge wa Mvomero, Jonas Van-Zeeland, alisema anafahamu changamoto ya ndovu hao na alishaiwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana lakini hawajapatiwa ufumbuzi.

"Miezi kadhaa iliyopita, majira ya usiku nilipigiwa simu na mheshimiwa diwani, nilikuja saa nne usiku, nikakuta mtu amekanyagwa tumboni, huwezi kumwangalia mara mbili.

"Sasa viongozi waliopewa dhamana wanafanya nini? Mimi mbunge, kazi yangu ni kusema, sina dola, sina chochote na ningekuwa na dola ningeweza kuwahamisha tembo, watu wa TAWA (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA)," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wakazi wa kijiji hicho, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema ataziwasilisha salamu zao kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana ambaye atafika na kutoa kauli kuhusu shida ya uvamizi wa ndovu kwenye makazi yao.

Alisema serikali imetekeleza miradi ya maji katika mikoa mbalimbali nchini na kuwafanya wananchi kuacha kutumia muda wao mwingi kutafuta maji na kuelekeza nguvu zao kwenye mambo ya kukuza uchumi.

"Sasa kinamama badala ya kupoteza muda mwingi kutafuta maji, mtautumia muda wenu katika shughuli za kukuza uchumi na baadaye kutulia na waume zenu majumbani mkipanga maisha, maisha yatakuwa raha kabisa," alisema.

Alimpongeza Mhandisi wa Maji Wilaya ya Mvomero, Sospeter Lutonjo kwa kutekeleza majukumu yake vyema na kuwa mhandisi wa mfano kwa kuwa Wizara ya Maji ilikuwa ya kero na lawama kwamba watu wanapewa pesa wakienda kukagua mradi haupo.

"Huyu amefanya kazi yenye kuonekana, Mungu ambariki sana, hata maandiko yanasema 'ukimaliza kazi unavalishwa taji', sasa umefika wakati wako wa kuvikwa taji, na huyu msije mkamhamisha mwacheni afanye kazi hii ambayo ameianza hapa Mvomero ili wananchi wa wapate majisafi na salama," aliagiza.

Naye Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Mvomero, Sospeter Lutonja, alisema kukamilika kwa miradi mipya yenye thamani ya Sh. bilioni tisa inayojengwa, kutawezesha kuongezeka upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Mvomero kwa asilimia 78 ifikapo mwezi Juni mwaka huu.

Lutonjo alisema mpango wa RUWASA ni kufikia asilimia 85 ya utoaji wa huduma ifikapo mwezi Desemba 2025, mwaka ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 - 2025.



Mkazi wa Kigamboni mkoani Dar es Salaam akiwa amepanda mkokoteni unaovutwa na punda akienda kutafuta maji jana. **PICHA: JUNANNE JUMA**

# Wajawazito walalama kutopewa huduma stahiki kwenye zahanati

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

BAADHI ya wanawake katika Kijiji cha Manga, Halmashauri ya Manispaa ya Singida wamedai kujifungua nje ya jengo la zahanati ya Kijiji hicho kutokana na huduma isiyo rafiki kutoka kwa watoa huduma wa zahanati hiyo.

Waliwasilisha malalamiko hayo wakati wa mkutano wa hadhara wa mbunge wa jimbo hilo, Mussa Sima aliyekuwa kwenye ziara ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji hicho, Saidoro Mangu, alidai kinamama wajawazito wanaokwenda kufuata huduma za kujifungua nyakati za usiku wamekuwa hawapati mapokezi sahihi kutoka kwa watoa huduma wa zahanati hiyo.

"Kutokana na kinamama hao kutopata mapokezi rafiki kutoka kwa watoa huduma wa zahanati hiyo wamekuwa wakijifungulia nje ya zahanati hiyo kutokana na watoa huduma hao kutowajali kinamama hao. "Hii inauma sana kwani mimi mwenyewe niliwahi kushuhudia tukio moja lililotokea katika zahanati hiyo la mama mjamzito kujifungulia nje ya zahanati kutokana na watoa huduma waliokuwapo kituoni hapo kutowajali wateja wao waliowaweka hapo," alidai.

Alisema kuwa wakati umefika kwa serikali ya wilaya hiyo kupitia kwa mwakilishi wa wananchi na Mkurugenzi kuangalia upya utendaji wa watoa huduma waliioko kwenye kituo hicho kwani inawezekana wamekaa muda mrefu na kujikuta wakitawaliwa na mazingira.

Aliyekuwa Diwani wa Mtipa, Saidi Chima alionyesha masikitiko yake kwa wananchi wa kijiji hicho kutoshirikishwa katika kufanya uamuzi wakati wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Alisema anafahamu kuna baadhi ya watu hawatakiwi kuonekana katika shughuli za maendeleo kwa madai kuwa anapinga maendeleo ya kijiji hicho.

"Kwa nini tupinge maendeleo, hatupingi tu maendeleo kwani tunahoji tujue kinachoendelea, kwani tungejua Sh. milioni mbili zimejenga ofisi na sisi tumepatiwa kiasi hicho cha fedha unafikiri kuna mtu angehoji? Chima aliuliza.

Akijibu malalamiko ya wananchi hao, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alikiri kupokea malalamiko hayo na tayari ameshamwandikia barua ya kumsimamisha kazi Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho hadi uchunguzi utakapokamilika.

"Na kwa sababu mimi ninasimamia ilaniyauchaguzi,kerohiimlivyosema, mimi nilishaletewa ofisini kwangu, na nilishamwita WEO (Ofisa Mtendaji wa Kata), na hatua nimeshachukua ya kumwandikia baru na kuanzia kesho hatakuwa hapa," alisema.

Mbunge Sima aliwaahidi wakazi wa kijiji hicho kwamba kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Manispaa, watatunda timu ya kwenda kuchunguza kama tuhuma za watoa huduma wa zahanati hiyo zina ukweli au la.

Mussa ambaye kitaalumu ni mwalimu, alisisitiza kwamba endapo timu hiyo itabaini kinamama wajawazito kutopatiwa huduma zinazostahili, serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria watoa huduma hao.

"Limejitokeza jambo kama hili kule Sokoine, sisi tumeliona kwenye vyombo vya habari, changamoto imejitokeza na timu imeundwa ya wilaya,Mkurugenziumeunda timu, timu imeundwa ya mkoa na timu imeundwa ya kitaifa.

"Tunatarajia ndani ya wiki hii tutapata majibu hatua zitakazochukulia katika hospitali yetu," alisema.

# Viongozi wa dini watoa neno ruhusa Rais vyama vya siasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini Mkoa wa Arusha, wamempa kongole Rais Samia Hassan Suluhu, kwa kuonyesha nia ya kukwamua mchakato wa Katiba mpya na kuruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara.

Akisoma tamko la viongozi wa dini mkoa huo, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, ambaye pia ni mwenyekiti wa viongozi hao, Dk. Stanley Hotay, alisema uamuzi wa kukwamua Katiba mpya ni jambo la muhimu kwa taifa.

Dk. Hotay alisema katika kipindi cha uongozi wa awamu ya nne, serikali ilianzisha mchakato wa Katiba mpya, wakati huo Rais akiwa Jakaya Kikwete ambaye aliunda tume kwa ajili ya mchakato huo ambayo ilikusanya maoni na kisha kupelekwa katika Bunge la Katiba.

"Tunapenda kuunga mkono hatua hii muhimu na adhimu iliyochukuliwa na Rais Samia kufufua mchakato huu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vile vijavyo katika taifa hili," alisema. Pia alisema wamefurahi kusikia katika kufufua mchakato huo, Watanzania wote na wadau wa sekta zote watahusishwa, hivyo wanaomba jambo hilo lifanywe mapema na kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi. Kuhusu mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, Askofu Dk. Hotay alisema makatazo yaliyotolewa awali yalisababishia athari hasi kwenye demokrasia na kuacha majeraha miongoni mwa vyama vya siasa na taifa kwa sehemu.

"Tunaunga mkono hatua hii ya Rais Dk. Samia kutoa ruhusa Januari 2, mwaka huu, kufanyika kwa mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu," alisema.

Aidha, alisema viongozi wa dini wanampongeza Rais Samia kwa kuendelea kutoa uhuru wa vyombo vya habari nchini kwa kuwa hilo nalo ni la muhimu kwa sababu kuna uhusiano mkubwa kati ya uhuru wa vyombo vya habari na maendeleo ya taifa lolote lile kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kidemokrasia.

Alisema Rais alipoingia madarakani aliahidi kuvifungulia vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa na kweli taifa na dunia imeshuhudia akitimiza ahadi yake.

"Kwa kuwa huu ni mwaka mpya, basi uwe ni mwanzo mpya. Tufunge ukurasa uliopita kama taifa na tufungue ukurasa mpya. Tujisahihishe pale tulipokosea na tusamehe waliokosa. Tumepewa mwaka huu kwa neema, hivyo tuutumie vizuri kama taifa.

"Tunatoa wito kwamba uhuru uliotolewa utumike kwa mujibu wa sheria, staha na kwa kuzingatia utamaduni wa Mtanzania na vyombo vya dola vitende haki sawa kwa wote. Vyombo vya habari visinunulike na waliopewa uhuru wautumie kwa manufaa ya kujenga wengine na taifa letu," alisema.




Naibu Mkurugenzi wa Halotel, Bui Van Thang, akikabidhi mfano wa funguo ya gari kwa mshindi wa gari, Scolastica Sostenes Haule (katikati), kutoka Mkoa wa Songea. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi wa Biashara, Abdallah Salum (Kushoto), mume wa Scolastika (wa pili kulia) na Naibu Ofisa Mkuu wa Fedha, Nagib Ferej. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshindi promosheni '7 bang bang' akabidhiwa gari

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mawasiliano nchini ya Halotel Tanzania PLC jana imemkabidhi mshindi wa promosheni ya 7 bang bang gari aina ya IST mpya.

Promosheni hiyo iliendeshwa kwa wiki 10 na kuwapa fursa wateja wote wa Halotel waliokuwa wakiwaunga mkono kwa kutumia huduma zao kwa miaka saba ya utoaji huduma bora za mawasiliano nchini.

Taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo jana, ilisema tangu kuanza kwa promosheni hiyo, zaidi ya washindi 140 wamejishindia zawadi mbalimbali zikiwamo vocha yenye thamani ya mpaka Sh. 100,000, simu janja na televisheni janja ya nchi 50. Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya gari hilo, Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum, alisema; "Leo hii, tuna mshindi aliyebahatika kujishindia gari jipya kwa kushiriki katika shindano letu la promosheni ya 7 bang bang. Tumeona itakuwa vizuri ikiwa zawadi hii ikakabidhiwa wakati tukiwa tunamalizia msimu wa sikukuu," ukiwa sambamba na kuwashukuru wateja wetu wote kutumia huduma za mawasiliano kutoka Halotel."

Akikabidhi gari hilo kwa mshindi Sholastika Sostenes Haule, alimpongeza na kumuasa kutumia zawadi hiyo ambayo ni fursa adimu, katika kupiga hatua kimaisha na isiwe mwisho wa jitihada zake na aendelee kupanda zaidi kimaisha.

Pia, aliwahimiza wateja wake waendelee kutumia mtandao wa mawasiliano wa Halotel unaoendelea kuwa na ubunifu kuhakikisha kila mteja anafurahia huduma za mawasiliano kwa ubora.

Sholastika aliishukuru kampuni ya Halotel na kuwasihi wateja kuendelea kutumia mtandao huo na kushiriki katika promosheni zinazotolewa kampuni hiyo ili waweze kujishindia zawadi mbalimbali zinatolewa kupitia promosheni hizo.

Pia kampuni hiyo ilifanya uzinduzi wa duka jipya na la kisasa Palm Village Mall, kando ya Barabara ya Mwai Kibaki Mikocheni, jijini Dar es Salaam kwa wateja kupata huduma zote zinazotolewa na duka hilo.

"Duka hili lililoboreshwa kwa njia ya kidigitali litatoa huduma zote zitakazojumuisha huduma ya kusajili laini mpya na kusajili upya namba za simu kwa mfumo wa alama za vidole, ubadilishaji wa laini kutoka 3G kwenda 4G, huduma za vocha (elektroniki na kukwangua) uthibitishaji wa namba za simu, huduma za HaloPesa, bidhaa za Halotel kama router na huduma zote za ziada na za baada ya mauzo," alisema.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Salum alisema mkakati wa Halotel ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja na kutimiza ahadi yake ya kuwapatia wateja fursa ya kupata bidhaa na huduma kwa ukaribu na urahisi zaidi.

"Tunapenda kuwakaribisha wateja na Watanzania wote kwa ujumla katika duka letu la Halotel hapa Palm Village Mall kuweza kupata na kufurahia huduma bora za Halotel katika duka hili," alisema.

# RAS Pwani ataka wanawake kununua hisa za kampuni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Pwani, Zuwena Omari, amelielekeza Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi mkoani hapa kuhakikisha linawafikia wanawake wa vijijini ili wajikwamue kiuchumi na kununua hisa kwenye Kampuni ya GoMama.

Omari alitoa maelekezo hayo jana mjini Kibaha wakati wa makabidhiano ya Kampuni ya GoMama yenye mtaji wa Sh. bilioni 50 kati ya serikali na Jukwaa la Uwezeshaji wa Wanawake kiuchumi Mkoa wa Pwani.

Alisema lengo kuu la kampuni hiyo ni wanawake kunufaika kwa mafunzo na kujiinua kiuchumi, hivyo ni jukumu la jukwaa hilo kuhakikisha linahamasisha wanawake kujiunga na majukwaa ya aina hiyo.

"Inatakiwa kuonekana athari ya kuanzishwa kwa jukwaa hili la wanawake ambao wako chini kabisa, wawe na mabadiliko na katika ununuzi wa hisa pia wanawake wa vijijini wanatakiwa wapewe kipaumbele," aliagiza.

Alisema kuwapo GoMama kuwe msingi wa wanawake kujifunza na kujiinua kiuchumi, akibainisha kuwa majukwaa 1,722 yaliundwa mkoani Pwani na 945 yalisajiliwa, hivyo yanatakiwa kuboreshwa zaidi na kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

Mtaalamu Mshiriki aliyeratibu uanzishwaji wa kampuni hiyo, Dk. Ramadhani Mwaiganju, alisema malengo ya kuanzishwa kwa kampuni hiyo ni pamoja na kuanzisha biashara zitakazosaidia wanawake kuinuka kiuchumi.

Dk. Mwaiganju alisema lengo lingine ni wanawake hao kutengeneza vifungashio na kuwa wakala wa kuuza vifungashio kutoka nje ya nchi kutokana na mkoa huo kuwa na viwanda vingi.

Alisema kampuni hiyo ina mtaji wa Sh. bilioni 50 sawa na hisa milioni 50 kwa kuwa kila hisa inauzwa Sh. 1,000. Alibainisha kuwa asilimia 60 ya hisa inatakiwa kufanyika uhamasishaji ili wanawake wanunue na asilimia 40 watauziwa watu wengine kwenye maeneo mbalimbali wakiwamo wanaume.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Pwani, Mariam Ulega, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha majukwaa hayo.

Mariam alisema kuwa baada ya kukabidhiwa kampuni hiyo, wanakwenda kuanza utekelezaji kwa kuwa na mbinu zitakazoendana na kasi ya Rais ikiwa ni pamoja na kuwafikia wanawake walioko Vijijini.

Mwenyekiti huyo alisema wanatarajia kutoa elimu kwa wanawake kuanzia ngazi ya vijiji kuhusu jukwaa na kampuni pamoja na ununuzi wa hisa ili wote wanufaike na kuwe na mabadiliko kiuchumi.



# Wadau wapongeza maboresho ya elimu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANUFAIKA wa miradi ya mfuko wa elimu katika mikoa ya Arusha na Manyara, wameipongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kuboresha miundombinu ya elimu katika maeneo yao.

Pia wamesema hali inachangia kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia katika maeneo hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Anna Mbogo, alisema mradi wa maabara ya sayansi katika Shule ya Sekondari Maganjwa, utainua ufaulu wa masomo ya sayansi katika shule hiyo kwa kuwa utawezesha wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mbogo alieleza hayo wakati Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alipotembelea miradi ya ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Sekondari Sokoni II na madarasa mengine matatu Shule ya Msingi Kaloleni za Jiji la Arusha.

Miradi mingine iliyotembelewa ni ya ujenzi wa matundu 24 ya vyoo katika Shule ya Msingi ya Kaloleni jijini Arusha, Shule ya Msingi Gidewari na Shule ya Sekondari Dareda za wilayani Babati, mkoani Manyara.

Pia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Seleman Msumi, alisema Mfuko wa Elimu umewezesha halmashauri yake kujenga madarasa matatu ya kisasa na kununua samani ambazo ni viti na meza.

Baada ya kuzuru miradi hiyo, Gauzye alisisitiza umuhimu wa shule zilizonufaika na ufadhili wa Mfuko wa Elimu, kutunza vyema miundombinu walizopata ili zidumu na kunufaisha wanafunzi wengi zaidi.

Mkurugenzi huyo alitembelea miradi sita ya ujenzi wa miundombinu ya elimu yenye thamani ya Sh. milioni 360 ambazo zimetolewa na Mfuko wa Elimu wa Taifa.

# Afungwa jela maisha kwa kunajisi kichanga

**Novatus Makunga,** ARUMERU

MAHAKAMA ya Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, imemhukumu John Sanare (23), Mkazi wa Kimnyaki wilayani hapo kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kubaka kichanga cha miaka mitatu na miezi miwili.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mahakamani hapo na Hakimu Mkazi Mkuu Gwantwa Mwankuwa, aliyekuwa akisikiliza shauri hilo.

Akisoma mwenendo wa kesi hiyo, Hakimu Mwankuwa alisema mshtakiwa Sanare ametiwa hatiani kwa kutenda makosa mawili ambayo ni ya ukatili dhidi ya mtoto na ubakaji.

"Mahakama hii imejiridhisha kuwa upande wa mashtaka umefanikiwa kujenga kesi hii na ushahidi uliotolewa haujaacha shaka yoyote.

"Kwa kuwa mahakama imejiridhisha kuhusu makosa haya, inatoa adhabu ya kifungo cha maisha jela ili iwe fundisho kwa wote wanaotenda ukatili kwa watoto katika jamii," alisema Hakimu Mwankuwa.

Makosa hayo ni kinyume cha kifungu cha 130 (1) 2 (e) na kifungu cha 131 (3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Penina Ngolea, kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 10, 2022 katika Kijiji cha Kimnyaki, wilaya ya Arumeru.

Nje ya Mahakama hiyo, wanaharakati wanaoongoza vita dhidi ya ukatili wa kijinsia, akiwamo Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Arusha, Beatrice Tengi, walieleza furaha yao baada ya mahakama hiyo kumtia hatiani mshtakiwa na kumpa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani.

"Pia tunapenda kutoa shukrani kwa jamii ambayo ililiibua suala hili na kulifikisha katika vyombo husika vikiwamo hospitali, polisi na mahakamani na leo (jana), hukumu imetoka," alisema.

Pia Ofisa wa Kitengo cha Kutetea Haki ya Mtoto kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Farida Masenika, alidai kuwa kwa sasa mwelekeo si mzuri ingawa alisema serikali iko macho kupambana na wote wanaofanya vitendo hivyo vya ubakaji wa watoto.

Alisema pia mahakama hivi sasa inafanyakazi kwa haraka, kwa kuwa kesi hyo imeendeshwa kwa miezi mitano pekee na haki imetendeka.



Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma (katikati), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi wa Usambazaji Maji Tanga-UWASA, Mhandisi Rashidi Shabani (wa pili kulia), juzi walipotembelea kukagua eneo linalojengwa mtambo wa kusafisha maji Magoroto. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Wazazi wampongeza Rais Samia kwa kuruhusu mikutano ya vyama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Taifa wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Fadhili Maganya, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa ruhusa ya kuanza kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini.

Pia amesema ziara za nje anazofanya Rais Samia, zina tija kwa kuwa akirudi nchini, harudi bure na zinafungua milango nje na ndani ya nchi. Maganya alisema hayo jana jijini hapo alipotoa tamko la umoja huo kuunga mkono uamuzi wa Rais Samia ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa CCM.

Alisema fursa ya mikutano ya hadhara iliyotolewa na Rais Samia ni kuonyesha namna bora ya kuendesha siasa hapa nchini.

Mwenyekiti huyo alisema Rais katika kuonyesha dhamira yake ya kujenga demokrasia, alisisitiza mikutano ya vyama vya siasa itumike kukosoa bila kugombana ikiwamo kuanza kukwamua mchakato wa Katiba.

Alisema pia Rais ameridhia kuendelea kuangalia sheria mbalimbali kwa ajili ya kuziboresha kwa maslahi mapana ya nchi na kuahidi ushirikishwaji wa wadau na makundi mbalimbali katika kuziboresha sheria hizo.

"Tunatoa wito kwa Watanzania wote kumtia moyo Rais Samia kwani umoja na mshikamano ndio msingi wa maendeleo katika nchi yetu," alisema.

Aliviomba vyama vya siasa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za siasa nchini ikiwamo kumuunga mkono kwa kuendeleza siasa za maridhiano kwa maslahi mapana kwa mustakabali wa nchi.

Kuhusu safari anazozifanya Rais Samia nje ya nchi, Maganya alitumia methali ambazo ni mgaagaa na mpwa hali wali mkavu, akisema mwenda bure si mkaa bure, hivyo Rais anaposafiri kuna fursa mbalimbali anafungua. Kuhusu mikopo wanayodai anakopa kopa sana, Maganya alisisitiza kuwa Rais anakopa kwa maslahi ya taifa na nchi kwa ujumla na mikopo inafanya kazi na kazi zinaonekana.



## DC aonya uchochezi shughuli maendeleo

**Na Anjela Mhando,** SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Thomas Apson, amesema hataki figisu wala janjajanja ya viongozi au wanasiasa wanaochochea wananchi wasishiriki shughuli za maendeleo katika wilaya yake.

Badala yake amesema anataka kuona wananchi hawachoki kushiriki shughuli za maendeleo kama ujenzi wa majengo matatu yanayoendelea kujengwa katika zahanati ya Naibili iliyoko wilayani hapa.

Mkuu huyo wa wilaya alisema hayo jana alipokuwa anazungumza jana na wananchi wa vijiji vinavyounda kata ya Makiwaru, wakati wa msaragambo wa ujenzi wa majengo ya zahanati hiyo inayotarajiwa kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya.

"Wananchi msichoke kushiriki shughuli hizi za maendeleo na sisi tutaendelea kuja kushirikiana na nyie kwenye hii miradi. Kwenye ujenzi huu, kadri siku zinavyozidi kwenda niwaombe tokeni sana na nyie msaidie kushawishi wenzenu waje, kwa sababu hii ina faida kwenu, hadi kwa wajukuu zenu.

"Nawaomba sana mjitokeze kwa wingi ili eneo hili liweze kupandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya. Wizara ya Afya, imeutengea mradi huo Sh. milioni 300, kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), nyumba ya mtumishi na maabara," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Upendo Mangali, alisema mradi huo ukifanywa vizuri kwa kuwa na majengo ya kisasa, haitakuwa zahanati tena, bali itakuwa kituo cha afya.

Pia Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Duncan Urassa, akizungumza kabla ya msaragambo huo, aliwasihi wananchi wa kata hiyo kujitahidi kuendelea kujitoa kwa moyo.

Diwani wa Makiwaru, Ezekiel Lukumay, alisema baada ya kupata miradi hiyo wananchi walishiriki ujenzi kwa kuleta malori 40 ya mawe na kuchimba kifusi.

# Dk. Shoo aonya watumishi kuhusu unafiki

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewanyooshea kidole watumishi wa umma na wanaofanya kazi kwenye taasisi za dini, kuacha kufanya kazi kinafiki kwa kuwa kufanya hivyo ni kuendelea kujenga jamii ya watu wanafiki.

Akizungumza jana na watumishi wa Dayosisi ya Kaskazini ya kanisa hilo yenye makao makuu mjini Moshi, Dk. Shoo alisema kuna tabia inaanza kuchipuka nchini ambayo bila kuipiga vita, jamii inaweza kujikuta inajengwa na watu wenye tabia ya unafiki.

"Tusifanye kazi kwa unafiki ila tufanye kazi kwa uaminifu ili kutimiza majukumu yetu. Hatupaswi kufanya kazi kwa unafiki au kufanya kazi kwa bidii eti kwa sababu fulani au mkuu wako anakuona.

"Tufanye kwa uaminifu tukijua tunawatumikia Watanzania wenzetu na taifa letu." Alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili, unafiki ni hali ya kujifanya kuwa rafiki ilhali ni adui. Ni hali ya kutokuwa mkweli. Mnafiki anaweza kupindisha ukweli kwa nia ya kujinufaisha, kujipendekeza au kumfurahisha mtu au kikundi cha watu.

Kuhusu dhuluma kwa wengine, Askofu Dk. Shoo alionya akisema: "Tusidhulumu katika kutega, tuzingatie muda, tusiibie kwa muda au kwa namna yoyote kwa maana neno la Mungu linatuambia adhulumuye atapata ujira wake.

"Ukimtumikia kwa uaminifu, ujira wako utabarikiwa. Mungu atusaidie kufanya kwa uaminifu, tukiombeana sisi kwa sisi ili Mungu atufanikishe na tuwe na Baraka," alisema Mkuu huyo wa KKKT.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo ya mradi wa maabara ya sayansi katika Shule ya Sekondari Magwanjwa Babati kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Anna Mbogo (kushoto), wakati wa ziara ya kutembelea miradi iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa katika wilaya hiyo mkoani Manyara . **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mradi wa bil. 40/- kumaliza kilio cha maji

**Na Hamida Kamchalla,** MUHEZA

MCHAKATO wa kumaliza tatizo la maji ya bomba katika wilaya ya Muheza mkoani Tanga, uko ukingoni baada ya serikali kutangaza mradi mpya utakaogharimu Sh. bilioni 40.

Vijiji vinavyotaabika kwa kero ya uhaba wa maji kwa miongo kadhaa sasa, vimeanza kupata matumaini baada ya Mbunge wa Muheza (CCM), Hamisi Mwinjuma, maarufu Mwana FA, kutangaza ujio wa neema hiyo.

Mbunge huyo aliwapa matumaini wakazi wa vijiji hivyo, alipokwenda kutembelea miradi ya maji inayotekeleza na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga (Tanga-UWASA).

"Kupitia mradi wa maji wa miji 28, serikali imetenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya Wilaya ya Muheza, kutatua kero ya upatikanaji wa maji. Tunataka upatikanaji wa maji ufikie asilimia 100.

"Mkandarasi tayari ameshabainі mahali ambapo yatawekwa matangi, kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo, na tunatarajiwa kwamba utekelezaji wake utaanza mapema mwezi Januari mwaka huu na utakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa," alisema. "Mji wetu unaongezeka pia tulikuwa na tatizo la majitaka lakini kule Kilapura, tuna mradi wa majitaka na tuna mfumo ule ule wa ukusanyaji majitaka. Tunaishukuru Wizara ya Maji, ilituletea Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kukusanya majitaka na mpaka sasa ujenzi uko asilimia 40," aliongeza.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga-UWASA, Rashid Shaban, akitoa maelezo kwa mbunge huyo, alisema miradi inayoendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Muheza, itasaidia kufikia asilimia 90 ya upatikanaji wa maji ifikapo Julai, mwaka huu.

Tumeshapata mkandarasi na sasa yuko kwenye hatua ya maandalizi. Muda si mrefu uchimbaji wa mtaro utaanza ili tuboreshe upatikanaji wa maji kutoka usambazaji wa mwendo wa lita za ujazo 1,500 kwa saa hadi lita za ujazo 2,000," alisema.

"Awamu ya kwanza, tuliotoa asilimia 34 lakini imetufikisha asilimia 65. Tumeanza awamu ya pili na tumelenga mpaka ikifika Julai, mwaka huu, tutoke hapa kwenye asilimia 65 tufike hadi asilimia 85.

"Na awamu ya tatu ya mradi, tunalenga tufikie asilimia 100 na kama siyo, basi angalau hata tufikie asilimia 95," alisema.




Ukurasa 17

Royal Tour iwe ni kazi endelevu, isisubiri matukio ndio tunaibuka



## RC Mrindoko: Katavi tunafunguka kwa kasi kona zote, barabara na madaraja

Ukurasa 15

BUFE
IJUMAA JANUARI 6, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Rais Ruto aweka wazi mtaji wa serikali, amtetea binti yake

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Kenya, William Ruto, juzi amezungumza na vyombo vya habari kuzungumzia masuala mbali mbali tangu kuchukua hatamu baada ya uchaguzi wa mwaka jana.

Pia, amemtetea binti yake, Charlene Ruto, kuhusu madai ya kuwepo kwa 'Ofisi ya Binti wa Kwanza." Tangu kuapishwa kwa baba yake mnamo Septemba, Charlene Ruto, amefanya hafla na mikutano kadhaa ya hadhi ya juu chini ya jina hilo.

Siku ya Jumatano, juzi Rais Ruto amekanusha kuwepo kwa ofisi hiyo, akitamka: "Mwacheni binti yangu Charlene, unajua hawa ni watoto, ni watoto tu, unajua kabisa kwamba hakuna ofisi kama hiyo... yeye ni bintiye William Ruto tu na wakati mwingine hajui mgawanyiko kati ya rais na baba."

Rais wa Kenya William Ruto amefichua kwamba alimuengua Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) wa Polisi, kutokana na visa vya watu kutoweka kwa lazima na mauaji ya kiholela.

Rais Ruto alikuwa amesema awali aliyekuwa mkurugenzi wa uchunguzi wa jinai George Kinoti, amejiuzulu.

Ruto aliambia wanahabari Jumatano usiku kwamba alikuwa na nia ya kuhakikisha hakuna mauaji ya kiholela yanayofanywa na polisi.



Rais William Ruto. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, akasema nchi hiyo haitashindwa kulipa deni lake licha ya changamoto kubwa za kiuchumi, akifafanua 'imefunga breki katika kukopa tena.'

Ilipofika Septemba mwaka jana, serikali yake ilisema itapunguza ukopaji wa gharama kubwa wa kibiashara kwa ajili ya vyanzo vya bei nafuu kama vile Benki ya Dunia.

Kama ilivyo kwa mataifa mengine kadhaa ya Afrika, kiwango cha mikopo cha Kenya kimekuwa katika hatari ya kupunguzwa kwa sababu ya deni linaloongezeka na viwango vya riba duniani kote.

Rais Ruto ametetea hatua yake ya kuagiza vyakula vilivyobadilishwa vinasaba (GMO), ili kuunga mkono hoja yake, Ruto alifichua kwamba vyakula vyote ambavyo nchi imekuwa ikiagiza kwa muda wote vina viambajengo vya GMO, lakini akasema viko ndani ya asilimia moja inayohitajika na ofisi ya kukadiria ubora wa bidhaa nchini Kenya (KEBS).

Ameongeza: "Siwezi kuhatarisha maisha ya watu walionichagua...mimi ni mwanasayansi, wanasayansi wote nchini wanakubaliana kwamba GMO haina madhara."

Kuhusu huduma zote za serikali kuwa za kidigitali ifikapo Juni; akinena zitawekwa katika mfumo wa kidijitali katika muda wa miezi sita ijayo.

Hayo yanajiri, huku serikali ikianza njia ya kujenga mapato ya ndani ili kujitegemea. Rais Ruto anasema, hilo pia linalenga kupanua wigo wa ushuru na wakati huo huo kuhakikisha mianya yoyote inayoletwa na makusanyo ya ushuru huo imezibwa.

***Kwa mujibu wa taarifa kimataifa.***

UCHUMI

# Wenyeji Shinyanga wanavyoondoa watoto shule, hadi shambani kila msimu wa kilimo

## • Yabuniwa faini 500/- kwa siku, kukomesha tabia hiyo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

DAIMA kila unapofika msimu wa kilimo, huwa inaelezwa kwamba, wazazi katika shule za vijijini huwazuia watoto wao kwenda shule, ili wakawasaidie shughuli za kilimo shambani, hapo suala la masomo hukatishwa kwa muda.

Hiyo inatokea, huku mkoa wa Shinyanga kuwa sehemu kubwa ya shughuli zake kiuchumi ni kilimo.

Mkoani hapa, wananchi hujishughulisha kwa asilimia kubwa na kilimo kila msimu unapofika, katika hatua ambayo inakinzana na kipaumbele cha elimu, ambayo huwazuia watoto wasiende shule, badala yake wakalime shambani pasipo kujali siku za masomo na umuhimu wa mahudhurio yake.

Masengwa ni kata iliyoko wilayani Shinyanga, ikiwakilisha maeneo mengi nchini, jambo ambalo wakulima huzuia watoto wao wasiende shule msimu wa kilimo, ili wakalime shambani na kuwa watoro.



Mwanafunzi, akiwa shambani akilima siku za masomo. **PICHA: MARCO MADUHU.**

**VIONGOZI SERIKALI**

Hussen Majaliwa, ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, anasema unapofika msimu wa kilimo watoto wengi huwa watoro hawaendi shule.

Anasema, ni kipindi cha kuanzia mwezi Januari mpaka Februari, ndio huwapo utoro mkubwa wa wanafunzi, wakishinda shambani kulima na wazazi wao, huku wakiyaacha masomo kwa muda.

Majaliwa anasema, baada ya kukithiri tatizo hilo la utoro wa wanafunzi, walikaa kikao pamoja na walimu wa shule ya msingi na sekondari ya Masengwa, wakajadili namna ya kuzuia utoro na kukubaliana kuwatoza fedha wazazi watoto wao wasipofika shuleni.

"Makubaliano ya kikao chetu, mzazi akimzuia mtoto wake kwenda shule ili akalime shambani, kwa mwanafunzi wa shule ya msingi anatozwa shilingi 500, sekondari 1,000 kwa siku moja," anasema Majaliwa.

**KUTOKA KIJIJINI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga, Zacharia Ntemi, anasema baada ya kupitisha adhabu hiyo ya kutoza fedha wazazi ambao watoto wao watakuwa watoro shuleni, waliitisha mkutano wa hadhara na kuwatangazia wazazi wote.

Anasema mpaka sasa wazazi ambao watoto wao ni watoro, huwa wanalipa fedha hizo moja kwa moja katika shule husika, iwe msingi au sekondari.

"Huku maeneo ya vijijini huwa tuna sheria kali, tukipitisha jambo letu, lazima litekelezwe. Hakuna wa kukaidi! Nenda shuleni ukaulize walimu kama fedha za utoro hazilipwi na wazazi na uhoji utoro umepungua kiasi gani," anasema Ntemi.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Masengwa, Twalah Swalehe, anasema kuwatoza wazazi fedha, kunasaidia kupunguza kasi ya utoro wa wanafunzi, kila unapofika msimu wa kilimo mahali hapo.

Anasema katika kipindi cha msimu wa kilimo, wanafunzi wengi huwa watoro na sababu ni wanaenda mashambani kulima na kupitwa na masomo.

"Kabla ya kuanza kutozwa wazazi fedha hizi za utoro mwaka jana, wanafunzi wengi hapa shuleni walikuwa watoro kuanzia asilimia 70 na kuna kipindi hua inafika hadi asilimia 90 wote wapo mashambani na wazazi wao wanalima," anasema Swalehe.

"Baada ya kubanwa kulipa fedha, utoro sasa hivi umepungua kwa asilimia 16 hadi 20, na fedha ambazo tunazipokea za utoro huwa zinakwenda kwenye maendeleo ya shule ikiwamo kununua taulo za kike, ili kuzuia pia utoro kwa watoto wa kike wanapoingia hedhi," anaongeza.

**MAOFISA ELIMU**

Ofisa Elimu wa Masengwa wilayani Shinyanga, Simon Charles, anasema faini ambayo wamepewa wazazi kulipa ni ndogo, sababu kuna utoro unaoendelea dhidi ya watoto wengi wanawaona wakilima shambani siku za masomo.

Katika kukabiliana na hali hiyo, anafafanua tayari wameshakaa vikao kujadili namna ya kuongeza faini hizo angalau ziwe kubwa, ili utoro usiwepo kabisa kipindi cha msimu wa kilimo.

"Fedha hizi za faini za utoro Shilingi 500 kwa shule za msingi na Sekondari Shilingi 1,000 wazazi wanaziona ndogo, na ndiyo maana hata ulipaji wake hauna shida na kuendelea kuwazuia watoto wao wasiende shule, japo siyo kwa ukubwa kama zamani," anasema Charles.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Masengwa, wilayani Shinyanga Atupokile Maseta, anasema jamii ya maeneo ya vijiji huwa ni vigumu kubadilika, kutokana na kupenda kuishi kwa mazoea wakiendekeza mambo ya kale, ndiyo maana licha ya kutozwa faini bado baadhi ya wazazi wanazuia watoto wasiende shule bali wakalime.

Anasema, licha ya kuendelea adhabu hiyo ya wazazi kutozwa fedha za utoro kwa wanafunzi, pia wamekuwa wakiendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa elimu na faida ya kusomesha watoto, ambao baadae watawasaidia kuwa tegemeo la familia na taifa.

Mwanafunzi, Tatu Lucas, anayesoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Masengwa, anasema kutozwa faini kwa wazazi wao, kumesaidia kupunguza kuzuiwa kwenda shule ili wakalime.

Mwanafunzi (jina linahifadhiwa), anasema wao watoto hawana sauti ya kuwagomea wazazi wanapowazuia kwenda shule sababu wao ni wakutii maagizo, lakini tangu ianze adhabu ya kutozwa fedha za utoro, haizuiwi sana kuhudhuria shuleni kama zamani.

"Ninaweza nisije shule labda siku moja na kwenda shambani, lakini kesho yake na kwenda shule nikiwa na Shilingi 500 mkononi kwa ajili ya kulipa faini ya utoro," anasema Amosi.

Mzazi, Juma Luhende, kutoka Masengwa wilayani Shinyanga, anasema baadhi yao huzuia watoto kwenda shule, ili wakalime sababu ya kupungukiwa na nguvu kazi na watoto ndiyo tegemeo lao, sababu bado wana guvu tofauti na wao umri umeshakwenda.

Akieleza suala la kutozwa faini ya utoro, anasema imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza utoro kwa wanafunzi, sababu kadri mtoto anapoendelea kubaki nyumbani na kiasi cha fedha kinazidi kuongezeka.

UCHUMI

# RC Mrindoko: Katavi tunafunguka kwa kasi kona zote, barabara na madaraja



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko.

**Na Neema Hussein, MPANDA**

KUKAMILIKA baadhi ya barabara mkoani Katavi, kumesaidia kuongeza fursa za kiuchumi na kurahisisha usafiri kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.

Kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Katavi kilichokaa hivi karibuni, kimejadili maendeleo ya mkoa kupitia miundombinu ya barabara.

Mgeni rasmi katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, anasema serikali imeendelea kuandaa bajeti na kuitekeleza ili kuhamasisha matengenezo ya barabara, ufunguzi wa barabara mpya, ukarabati na ujenzi wa madaraja unaendelea kufanyika.

Anasema, ujenzi wa barabara za kitaifa nao umeendelea kwa kiasi kikubwa ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 mkoa wa Katavi ulipokea bajeti ya shilingi bilioni 11.7 na mwaka 2022/2023, wamepokea bilioni 12.7 itakayo tekeleza miradi 39 ya barabara.

"Ndugu viongozi wa kikao hiki cha bodi ya barabara nitaje miradi michache ya kitaifa ambayo imefanyika ndani ya mkoa wetu wa Katavi ikiwa ni mafanikio makubwa ya kuufungua mkoa wetu wa Katavi kiuchumi,kibiashara, kihuduma za jamii na kimawasiliano.

"Tunayo barabara yetu ya kuelekea Uvinza Kigoma, ambayo tayari tumeishapata kilometa 35 na sasa tuna mkandarasi ambae yuko saiti tayari kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 25 za kiwango cha lami.

"Kazi ya mkandarasi huyo imeanza mwezi Julai 2022 na gharama za mradi huo zitakua shilingi bilioni 35.6 ambazo zitatekelezwa kwa kiwango cha lami kuanzia Vikonge kuelekea Ruhafwe. Naomba makofi mengi sana kwa mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuunganisha mkoa wetu na mikoa jirani.

"Pia, mtakumbuka tulikuwa na barabara ya Mpanda-Stalike ambayo ilikamilika na inatumika na sasa tunayo barabara nyingine ambayo inatokea Kibaoni-Stalike na kwa sasa itaishia eneo la Mlele 'junction' (makutano) na barabara hiyo ina urefu wa kilometa 50 na itajengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 81.7 na tayari utekelezaji unaendelea.

"Makofi mengi sana kwa mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuunganisha pia upande huo kwa kuelekea mkoa wa Rukwa," anasema Mrindoko, kisha anaendelea:

"Vilevile ndugu viongozi pamoja na wajumbe wa kikao cha Bodi ya Barabara (Katavi) tunayo barabara yetu nzuri sana ya Mpanda-Tabora kilomita takribani 337.4, ambayo utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 99 na hiyo asilimia moja iliyobaki ni ya kipindi cha matazamio ambao sisi watu wa kawaida tunasema imekamilika kwa asilimia 100.

"Nina hakika barabara hiyo imetufungulia sana uchumi wa mkoa wetu wa Katavi na kuendelea kutuhakikishia ukusanyaji wa mapato, utoaji wa huduma, usafirishaji wa mbolea, usafirishaji wa mazao na ushirikiano mbalimbali unaendelea kukua kwa sababu ya kufunguka kwa mkoa wa Katavi kuelekea makao makuu ya nchi Dodoma, kupitia Tabora."

HALI YA M ADARAJA

Mkuu wa Mkoa anataja hali ya madaraja makubwa, ambayo yanaendelea kujengwa huku akitolea mfano daraja linalojengwa katika Halmashauri ya Mpimbwe litakalogharimu shilingi bilioni 4.9 ambalo ujenzi wake unaendelea, kuunganisha wananchi wa vijiji mbalimbali katika halmashauri hiyo ili kuondoa changamoto waliyokua wakipata katika mto Msadya.

"Tukija kwa upande wa TARURA, bajeti ya mwaka 2021/2022 ilikua bilioni 15 na mpaka kufikia mwisho wa mwaka tulikuwa tumepokea zaidi ya bilioni 11 ambazo zimetekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungua barabara mpya, kufanya ukarabati wa barabara, kujenga madaraja pamoja na makaravati na kuhakikisha barabara zetu za vijijini zinapitika kwa kipindi chote cha mwaka," anasema.

Kwa upande wa TARURA, bajeti ya mwaka 2022/2023 ni bilioni 14.29 na sasa miradi yote iliyokusudiwa mikataba yake imesainiwa na kazi inaendelea kuhakikisha barabara zinapitika.

**KUTOKA TANROADS**

Martine Mwakabende, ni Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoa wa Katavi, anasema katika mwaka wa fedha uliopo, wanategemea kuweka taa za barabarani urefu wa kilometa tano katika eneo la Magula, Stalike, Majimoto, Inyonga na Mpimbwe.

"Barabara ya Mpanda -Tabora imekamilika kwa asilimia 100 zoezi ambalo linaendelea sasa hivi ni iko katika kipindi cha maandalizi ya mwaka mmoja.

"Tuna jukumu la kudhibiti magari mazito kwa kuyapima yakiwa na mizigo na yakibainika yamezidisha mzigo tunayatoza gharama za uharibifu kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani.

"Tuna changamoto nazo ni baadhi ya wananchi kupitisha mifugo barabarani na kuchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa barabara, wananchi kufanya shughuli za kilimo maeneo ya hifadhi za barabara mfano barabara ya kwenda Karema, Majimoto kuelekea Kasansa.

"Changamoto nyingine fedha inayotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutokidhi mahitaji halisi ya ukarabati wa barabara,uharibifu wa vyombo vya usalama barabarani kunaongeza gharama za matengenezo ya barabara na kuhatarisha usalama wa watumiaji wa barabara.

"Naomba niitarifu tu bodi yako miezi miwili mitatu hapo nyuma tulipata changamoto ya baadhi ya wananchi wasio na nia njema na serikali hii walizikata taa tatu za barabarani maeneo ya Misunkumilo kwa nia ya kuziiba na kuchukua chuma chakavu.

"Kabla hawajaondoka nazo kupitia kwa askari jamii wa eneo hilo walitoa taarifa na tukawahi kuzibaini,pia kuna changamoto ya uhaba wa upatikanaji wa vifusi hususan kwenye barabara zinazopita katika maeneo ya hifadhi kutokana na sheria kutoruhusu kuchukua vifusi katika maeneo ya hifadhi," anasema.

Wajumbe waliohudhuria kikao hicho wameishauri TARURA kwa mujibu wa sheria za barabara, watoe maelekezo yapelekwe polisi ili kuzuia magari makubwa kwenda vijijini kutokana na barabara za huko kutokuwa na uwezo wa kuhimili uzito wa magari hayo.

**NENO LA MBUNGE**

Mbunge wa Viti Maalumu, Taska Mbogo, anatoa maoni yake kwa kukazia swala la barabara ya Karema kilometa 112 kwa kiwango cha lami ambapo anasema.

"ujenzi wa barabara hiyo ni muhimu sana kwa sababu serikali imetoa pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi wa bandari kule Karema na barabara hiyo isipojengwa kwa kiwango cha lami inamaana ile bandari itakua hamna mizigo mizito itakayopita kwenye ile barabara na kwenda kwenye bandari yetu ya Karema,"anaeleza mbunge huyo.



Moja ya barabara mpya zilizojengwa mkoani Katavi. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

UCHUMI

MABADILIKO YA TABIANCHI...

# Maelekezo ya FAO: Mtama mbadala rasmi msimu shambani kukabili harufu ya njaa

**Na Christina Mwakangale**

NCHI zilizopo ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania, tegemeo la kiuchumi liko kwenye kilimo, kwa kuwa robo tatu ya wakazi wao, wamejikita katika kilimo.

Tanzania inaitegemea sekta hiyo katika ukuaji uchumi na maendeleo ya wananchi, huku ikitoa ajira kwa asilimia 61.1 ya nguvu kazi ya Watanzania, ambao aidha wamejiajiri moja kwa moja kwenye sekta hiyo au kupitia mnyororo wa mazao ya kilimo.

Mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kwenye nchi mbalimbali duniani, imekuwa sababu ya ukame, mabadiliko ya hali ya hewa, mafuriko, njaa, joto au baridi kali, kina cha maji kuongezeka baharini achilia mbali vimbunga na matukio ya moto katika milima na misitu ya asili.

Shirika la Chakula Duniani (FAO), limeutangaza mwaka huu kuwa mwaka wa zao la mtama, likisema ni fursa ya kuongeza ufahamu na kuelekeza umakini wa kisera kwa manufaa ya lishe na afya itokanayo na zao hilo, kutokana na hali mbaya ya hewa.

Awali, viongozi wa nchi zipatazo 100 walikutana nchini Misri, ikiwa ni kuendeleza juhudi za kimataifa za kukabiliana na ongezeko la joto duniani linaloambatana na mabadiliko ya hali ya hewa kwenye mkutano uliojulikana COP27.

Hadi sasa ni zaidi ya miaka sita, tangu kutiwa saini Mkataba wa Paris, kupunguza ongezeko la joto duniani hadi nyuzi joto 1.5, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akisema mkutano wa hali ya hewa wa COP27, lazima utoe 'malipo ya awali' kusaka majawabu ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi na yalingane na viwango vya ukubwa wa tatizo.

**TATHMINI MPYA**

Pia, kuna mzigo mwingine unaoliangukia bara la Afrika, hususan zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ingawaje Asia nayo inaguswa. Tathmini ya wiki iliyopita kuhusu uchumi wa dunia kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), inasema:" Mwaka 2023 utakuwa wa mdororo wa uchumi."

Shirika hilo linaloshughulikia utulivu wa uchumi wa dunia, limetabiri hali ya ukuaji uchumi ujao, kutokana na matokeo ya mgogoro wa kati ya Russia na Ukraine, likisema nchi zinaweza kupunguza maumivu mwaka huu, ikiwa zitafanya kazi pamoja.

IMF inasisitiza kwamba mataifa makubwa ya kiuchumi yaendelee na juhudi zao za kupunguza gharama ya maisha, hata kama yataathiri ukuaji wa uchumi.

**FURSA ZA MTAMA**

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazolima zao la mtama, huku FAO ikisema mwaka huu pia utachagiza uzalishaji endelevu wa mtama, ukiangazia uwezo wa zao hilo wa kutoa fursa mpya za soko endelevu kwa wazalishaji na watumiaji.

"Huku mifumo ya kimataifa ya chakula cha kilimo ikikabiliwa na changamoto za kulisha idadi ya watu inayoongezeka duniani kote, nafaka zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi kama mtama hutoa chaguo la bei nafuu na lenye lishe bora na juhudi zinahitajika kuongezwa ili kukuza kilimo cha zao hilo," shirika hilo linasema.

**AINA ZA MTAMA**

Katika ujumbe maalum wa mwaka wa kimataifa wa mtama, FAO inataja kuwapo aina mbalimbali za mtama, zikijumuishwa kwa majina; lulu, seredo, mkia wa mbweha, uwele, ulezi, serena, macia, teff, pamoja na fonio au mtama mkubwa.

Mtama ni chanzo muhimu cha lishe kwa mamilioni ya watu katika maeneo ya Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia. Na zao hilo limejikita sana katika tamaduni za watu asilia na kusaidia kuhakikisha uhakika wa chakula katika maeneo ambayo yana umuhimu wa kitamaduni.

Mkurugenzi Mkuu wa FAO, Qu Dongyu, anasema: "Mtama ni moja ya mazao ya ajabu ya kutoka kwa mababu zetu yenye thamani ya juu ya lishe na mtama unaweza kuwa na jukumu muhimu na kuchangia katika juhudi zetu za pamoja.

"Itawawezesha wakulima wadogo, kufikia malengo ya maendeleo endelevu, kuondoa njaa, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kukuza bioanuwai, na kubadilisha mifumo ya chakula ya kilimo."



Zao la mtama katika hatua tofauti za ustawi shambani.

Anafafanua kuwa uzalishaji mkubwa wa mtama unaweza kusaidia maisha ya wakulima wadogo na unaweza kutoa ajira zenye staha kwa wanawake na vijana.

"Mwaka huu wa kimataifa wa mtama ni ukumbusho wa umuhimu wa zao hili na unatoa fursa ya kipekee ya kuongeza ufahamu wa zao hilo. Mwaka 2023 kuwa mwaka wa mtama duniani, ulipitishwa na kutangazwa katika kikao cha 75 cha Baraza Kuu Machi 2021 na FAO ndio inashika usukani wa mwaka huu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali."

**WADAU WANENAVYO**

Hivi karibuni, Kampuni ya Pass Leasing na kampuni ya Mobikey watengenezaji wa matreka waliingia makubaliano ya ukopeshaji na kukodisha zana za kilimo kwa wakulima.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Pass, Killo Lusewa, anasema wanufaika wa makubaliano hayo ni sekta ya ufugaji, uvuvi, mazao ya misitu na viwanda.

"Mtu binafsi, kikundi, chama na kampuni wanaweza kupata zana hizi bila dhamana na kwa masharti nafuu sana, ili kukuza mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo," anasema Lusewa.

**UWEZESHAJI**

Wakulima wa mtama kwenye wilaya sita za mkoa wa Dodoma, zilinufaika na mradi wa kilimo himilivu cha zao hilo (CSA), unaosimamiwa na Shirika la Farm Africa na kuwezeshwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

Kwa mujibu wa WFP, wakulima hao katika msimu wa mwaka 2020/2022 wamevuna tani 28,000 za mtama uliowaingizia Sh. bilioni 13.5.

Mkuu wa Ofisi Ndogo ya WFP ilivyopo Dodoma, Neema Sitta, amesema mradi huo umeleta tija kubwa kwa wakulima ambao kwa sasa mbali ya kuvuna mtama mwingi, pia wamekuwa na soko la uhakika na kuondoa changamoto ya soko kwa zao hilo.

"Mradi wa CSA unatekelezwa katika vijiji zaidi ya 200 vilivyopo kwenye wilaya sita za Mpwapwa, Chamwino, Bahi, Kongwa, Chemba na Kondoa kwa msimu wa mwaka 2020 hadi 2021.

"Mradi huu ni wa gharama ya shilingi bilioni 1.7 na umegusa wakulima zaidi ya 22,000 ambao wapo kwenye mradi kutoka katika wilaya hizo, umenufaisha ya watu 100,000 ndani ya Mkoa wa Dodoma," alisema Neema.

**ZAO LINAKOUZWA**

Januari mwaka 2021, Kampuni ya Bia Tanzania (TBL Plc), imeongeza makubaliano ya kushirikiana na WFP katika mradi wa pamoja wa kuendeleza zao la mtama msimu wa mwaka 2021.

Mradi ulishirikisha wakulima 4,000 ambao walitarajiwa kuzalisha tani 10 za mtama na TBL Plc kukubali kununua mtama huo, kwa bei ya Sh. 550 kwa kilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Philip Redman, anasema mradi wa mwaka 2021, ni mwendelezo wa mradi wa pamoja wa majaribio uliopata mafanikio makubwa kwa kuongeza mavuno kwa asilimia 70 zaidi ya mwaka 2020.

Anasema, pia mradi wa majaribio ulilenga kufanya kazi na wakulima 2,000 kwa kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa, namna ya kuboresha mavuno na ubora wa mtama sambamba na kuwapatia soko la uhakika la mazao watakayozalisha.

Mmoja wa wakulima wa mtama ambaye pia ni kutoka Katibu wa Kikundi cha Wakulima wa mtama Kijiji cha Sagara B wilayani Kongwa, Theodora Mgaya, anasema mafunzo ya matumizi ya teknolojia yanawajengea uwezo.

Kwa mujibu wa TBL Plc, hununua asilimia 74 ya malighafi zake nchini na imedhamiria kuongeza manunuzi ya malighafi ndani ya nchi katika kipindi cha miaka ijayo.



Mtama uliovunwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Royal Tour iwe ni kazi endelevu, isisubiri matukio ndio tunaibuka






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

TUMESHAUANZA mwaka mpya na sasa tugange yajayo. Mimi naendelea kutafakari tulikotoka, tuliko na twendako, hasa nikizingatia kuwa kazi inaendelea katika taifa hili lenye mambo mengi.

Natafakari alichokifanya Rais Samia Suluhu Hassan kwa nchi hii kupitia filamu yake ya The Royal Tour na kinachoendelea kwa sasa, nakuna kichwa mpaka kinaniuma.

Naona kama wahusika wamemtelekezea jambo hilo, ambalo hakika kama tungelibeba itakiwavyo, bila shaka nchi hii ingetangazika kimataifa na manufaa yake yangeonekana dhahiri.

Limenijia hilo, baada ya juzikati hapa kuona video ikimwonyesha Nick Reynolds almaarufu Bongo Zozo, yule Mwingereza aliyeamua kututangazia nchi kwa mapenzi yake na nadhani hata bila malipo, akiwa mtaa fulani ughaibuni akiwa na bendera ya Tanzania.

Zozo anafika mahali anaulizia Wazungu wenzake watambue ile ni bendera ni ya wapi, hakuna anayeitambua hata licha ya kuwaambia ni ya nchi yenye Mlima Kilimanjaro, ndipo kwanza anaibuka mmoja na kusema kwa kujiamini kuwa ni bendera ya Kenya!

Inauma sana kusikia kuwa bado kuna watu wanaamini Mlima Kilimanjaro uko Kenya, licha ya juhudi zilizofanywa na Rais katika filamu yake, kumbe ikaonekana baada ya uzinduzi kuendelea kulitangaza Taifa na vivutio vyake, si kwa kasi inayostahili hata kidogo.

Natazama tulivyo na midege mikubwa tuliyoipokea kwa bashasha na nderemo, lakini tumeiacha na rangi ya bahari siku zote, huku kukiwa na fursa ya kuzichora hata vivutio vya nchi hii vikatangazika ndani na nje ya nchi.

Tunatangaziwa kuwa midege hiyo itakuwa ikifanya safari za masafa mpaka Mashariki ya Mbali; China, ambako lazima kuna watalii ambao kama zingekuwa zimechorwa wale wanyama watano wakuu-Big Five na Mlima Kilimanjaro, tungetangaza.

Lakini leo tunaziona ndege zikiruka na rangi ile ile ya siku zote, isiyo na matangazo yoyote, zaidi ya 'Hapa Kazi Tu', ambayo kwa wageni hawawezi kujua hayo maneno yanamaanisha nini au ni kivutio cha nini mpaka kivutie!

Nilipata kusema huko nyuma, kuwa Watanzania tunashindwa kutangaza utamaduni na vivutio vyetu vya kijadi hata kuvutia watalii, kwa sababu tumejikuta tukitekwa kifikra na mambo ya kigeni.

Mathalan, hivi ni mtalii gani anataka kuja Tanzania kuangalia hoteli ambazo hata kwao zipo? Nani anataka kuja kula vyakula ambavyo hata kwao uzunguni vipo?

Tunashindwa nini kuwa na vijiji vya kitalii, vyenye vivutio vya kijadi, kama nyumba za tembe za msonge na kadhalika, ambako watalii watapenda kulala ili kubadilisha mazingira badala ya hoteli za nyota tano au sita walizoziacha kwao?

Tunashindwa nini kuwalisha ugali kwa kisamvu, mlenda, mgagani, maboga na kadhalika badala ya mbatata na kuku wa KFC, ambavyo kwao wanavila na kusaza na hivyo kuja kwao huku ni kutaka kubadilisha mazingira, vyakula na hata malazi.

Kana kwamba haitoshi, leo hata muziki wa Kitanzania hakuna, akija mtalii akifika mahali anakotaka kupumzisha akili, atasikiliza muziki wa kwao ule ule! Wanaoitwa wanamuziki wa Kitanzania hawapigi wala kuimba muziki wa Kitanzania, bali wa kuiga, wa kigeni.

Tena ndiyo kwanza utasikia msanii anajiita '... Boy', akitamba kuwa anaimba muziki wa Kitanzania, lakini akijinasibu kuwa kuanzia sasa ataimba nyimbo za Kiingereza tu! Huyu anatangaza utamaduni wa nchi kweli au Tumbo Street?

Mwingine anajiita lake, tena afadhali angejiita madini fulani ya thamani, naye anaimba nyimbo za Kinaijeria kama si Kizulu, lakini utasikia naye anasema anaimba muziki wa Kitanzania! Tanzania ipi? Ya Afrika Kusini au ya Afrika Magharibi?

Juzi kuelekea kufunga mwaka 2022, kuna maeneo fulani ya burudani ndani ya Dar es Salaam yenye jina linaloendana na maisha ya baharini, ikaandaa tamasha la muziki.

Kilichoonekana hapo ni watoto wa kike waliovalia nusu uchi wakicheza hadharani bila ya aibu wala soni. Hao nao tutasema wanatangaza muziki wa Kitanzania, ambao utavuta wageni kutoka huko waliko kuja kushuhudia, kweli?

Hakika ule ulikuwa ni muziki wa Karibiani. Hivyo akija mgeni kutoka visiwa hivyo vya Kusini mwa Amerika, hatasumbuka kuuangalia kwani ndio muziki wa kwao. Kuna watu nasema kila siku na kila mara, kwamba wamepewa dhamana ya kuulinda na kuuendeleza kama si kuutangaza utamaduni wa kitanzania sambamba na vivutio vilivyoko nchini, lakini hakuna wanachifanya zaidi na wao kutekwa na mambo ya kigeni, ukiwaulizia Singeli watakutazama kama mtu wa za gani vile.

UCHUMI

# Kamanda Muliro: Pikipiki zinazojizima zinaturahisisishia kazi, bajeti kudaka wezi

## •Waendesha bodaboda Dar washangilia...




Baadhi ya madereva wa bodaboda wakiwa kazini mkoani Singida, wakiwa na vazi 'reflector' inayohimizwa na serikali kwa ajili ya utambulisho **PICHA: HALFANI CHUSI.**

**Na Halfani Chusi**

ALHAMISI wiki iliyopita, gazeti hili liliibua kuwapo namna ya kukabili uhalifu wa wizi wa pikipiki, ikiweza kumdhibiti anayeiba katika kumnyima ushirikiano wa 'kuwaka moto'.

Hata hivyo, aina hiyo ya ubunifu uliowekwa na kampuni ya biashara ya pikipiki ya TVS kukabili katika namna moja au nyingine ya shughuli hiyo, kuna mambo mawili makuu ndani yake; usalama wa umma na mali zao, pia kuimarisha uchumi wao.

Kikuu hasa katika hilo ni kwamba, suala la usalama wa raia wake na msimamizi mkuu wa ulingo huo wa kiusalama, msimamizi mkuu ni Jeshi la Polisi.

Kwa kuwa, Dar es Salaam ni eneo mojawapo ambalo matukio ya wizi yanafanyika zaidi, Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi kanda maalum ya Dar es Salaam kupata maoni yake.

Kimsingi, ni mfumo wa teknolojia mpya kisasa, ambao asiye mmiliki wa pikipiki hawezi kuiwasha na kuondoka nayo, pasipo baraka za mmiliki wake.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, katika mazungumzo yake na Nipashe juzi, akiwa katika uso unaotabasamu na hulka ya kupigia makofi mageuzi hayo na ugeni wa mwanahabari kutambua nafasi ya chombo chake, akifafanua kwa lugha iliyojaa mifano:

"Utaratibu wa kuweka mfumo wa kuipata pikipiki inapoibiwa kwenye pikipiki ni jambo zuri sana, kampuni hiyo (TVS) inatusaidia kulipunguzia Jeshi la Polisi gharama, pamoja na muda wakati wa kutafuta chombo kilichoibiwa.

"Mfano, pikipiki imeibiwa Mbagala, mkija kuiangalia kwenye mfumo inaonekana ipo Manzese, sasa kwa nini muende Mbagala wakati pikipiki inaonekana Manzese?"

Anaendelea:"Kwa hiyo, mnatoka hapa mnaanza kuifuatilia, mara nyingi huwa tunakuta mtu keshaibwaga kwenye pagale,



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro. **PICHA: MTANDAO.**

halafu kakimbia. Kwa hiyo, sisi pale tunachukua pikipiki halafu tunaanza kumtafuta mwizi.

"Lakini tayari mali ya mmiliki inakuwa imepatikana. Sisi tunaendelea kumtafuta mwizi kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali pamoja na raia wema.

"Ninachoweza kusema hiyo ni teknolojia ya kisasa nzuri ya kupambana na wezi na sisi Jeshi la Polisi, tuko macho usiku na mchana kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao uko salama."

Mengi Japhet, mwendeha bodaboda wa eneo la Mabibo, Dar es Salaam, anasema: "Maboresho ya ulinzi kwa pikipiki ni ukweli usiopingika... wako vizuri na wamefanya maboresho makubwa sana, kwa mfano kwenye mafuta huko ndio usiseme yaani inanusa tu."

"Madereva wengi tunataka faida, yaani tutumie mafuta kidogo, lakini tupate faida zaidi, ukiweka lita moja kwenye TVS unapata kipato kikubwa kuliko mtu anayetumia pikipiki nyingine.

"Mimi nimesha endesha pikipiki nyingi, tena za kampuni tofauti tofauti lakini kwa habari ya kula mafuta kiduchu TVS kwangu mimi naona wako vizuri katika hilo," anasifu.

Bodaboda mwingine, Noeli Kilongosi, kutoka maeneo ya Bunju, anaungana na mtangulizi wake kwenye kuimwagia sifa kampuni hiyo akidai kwa sasa ni habari ya mjini akitamba kufurahia huduma hiyo.

"Zamani wakati inaingia mjini ilikuwa inaonekana kama ni pikipiki fulani hivi ya kawaida lakini kwa sasa kila mtu anatamani kuwa nayo, watu wengi kwa kipindi hicho hawakuipenda kwa sababu spea zake zilikuwa zinapatikana kwa shida.

"Sasa hivi, kila kona 'spea' zinapatikana na mafundi wapo wengi wazuri na wengine wamepewa mafunzo kutoka kwenye kampuni yenyewe. Hata soko lake lilikuwa dogo ukiitumia unapotaka kuiuza hupati mteja kirahisi kama ilivyo kwa sasa," anasema.

Kilongosi anasema hali inayowapa faida hata kuizuia pikipiki iliyotumika. Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam Maiko Massawe, anataja ni teknolojia inayowapa tabasamu, kama ilivyo kwa Kamanda Muliro, akipongeza pia aina ya kofia zao. Anasema: "Mimi kama kiongozi nilikuwa napewa sana lawama na madereva ninaowaongoza kwenye mkoa wangu, wengi walikuwa wanalalamikia kofia ngumu (Helmet) hazina ubora.

"Kwa hiyo, tunachohitaji kwa sasa hata kampuni nyingine zinazozalisha ziige ili kuwanusuru madereva wa pikipiki pindi wanapo pata ajali."

Meneja wa Mauzo wa Kanda kutoka kwenye Kampuni ya TVS Razaki Kasanga, alipopigiwa simu na Nipashe kujibu hoja hizo, akasema: "Kampuni yetu kitu namba moja inachokifanya ni kusikiliza wateja na kuyafanyia maboresho maoni yao."

"Lakini jambo jingine ambalo tumeliongeza kwenye kampuni yetu, kuna kifurushi kinaitwa 'Rider Cover' ambacho endapo dereva kwa bahati mbaya akapata ajali na akapata ulemavu wa kudumu au kufariki, anaweza kulipwa hadi milioni tano, lakini awe na leseni iliyo hai pamoja na ripoti ya polisi," anaongeza na kuhitimisha:

"Wengi wao wanapokuja ofisini kwetu kununua pikipiki tunawashauri wakate bima hiyo, ili wawe salama wanapokuwa pindi watakapo pata ajali....Wale waliobahatika kuelewa kiukweli wanakata bima na wanafurahia maisha kwa dereva bodaboda hakuna kitu kizuri kama kujiwekea kinga ya maisha kwa sababu hiyo itakuwa kwa faida yake mwenyewe."

***Pata simulizi ya 'Panya road' UK. 19.***

UCHUMI

# ... Kamanda Muliro afunguka vita vya 'watoto kujiajiri' kwenye 'panya road'

**Na Halfani Chusi**



Washukiwa wa 'Panya Road' wakiwa chini ya ulinzi. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

JE, ni namna gani Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, kupitia kiongozi huyo limefanikiwa kuteketeza vikundi vya kihalifu na watoto 'kujiajiri' 'panya road'? Ni swali ambalo Nipashe iliamshia mada kwa Kamanda Muliro kupata kujua undani uliopo?

Kamanda Muliro anasema 'panya road' ni wakongwe na hawajaanza sasa, walikuwapo tangu muda mrefu, lakini wanatumia majina tofauti kutisha jamii.

Anarejea historia, vikundi hivyo vya kihalifu vilianza mwaka 1990 kwa jina la 'mbwa mwitu, mwaka 2005 walikuwa wanajiita 'kiboko mashine; mwaka 2009 walikuwa wanajiita watoto wa mbwa; mwaka 2013 wakawa na jina Kumi Ndani Kumi Nje; mwaka 2017 walikuwa wanajiita Komando Yoso; mwaka 2022 wakaja na jina Panya Road.

"Kama nilivyovitaja vikundi, unaona ni kwa namna vilivyokuwa vinasumbua kila siku vinakuja na majina mapya lakini ukiangalia wengi wao wale vijana waliolelewa na mzazi mmoja.

"Wengine ni wale wasio maliza shule na kujiingiza kwenye tabia ambazo zipo kinyume na maadili, ndio maana jeshi hili kwa sasa limeanza pia kutoa elimu ya mfumo wa malezi kwenye familia, pamoja na shuleni waliko wanafunzi.

Kwa mujibu wa Kamanda Muliro, wengi wao wako katika umri wa kusoma darasa la nne hadi nafasi ya kusoma kidato cha pili, akifafanua kuwa, polisi inaamini wazazi wakipatiwa elimu ya malezi na watoto mambo yatakuwa mazuri.

Pia, mbinu za kujiepusha na tabia hatarishi kwenye jamii, ni muhimu na kuna uwezekano mkubwa kumaliza kabisa kuibuka tabia ya vikundi vya kihalifu.

"Ili kukomesha kabisa vitendo hivyo jamii inapaswa kuungana na kuwa kitu kimoja, elimu itolewe kwa wazazi, taasisi za dini, misikitini, shuleni kwa sababu suala la kukabiliana na vitendo vya kihalifu sio suala la kuliachia jeshi la polisi pekee," anafafanua.

Vilevile anasema, polisi imefanikiwa kupunguza matukio ya wizi wa pikipiki kwa kiasi kikubwa, akibainisha ndio njia walizozitumia kwa madereva bodaboda.

"Tuligundua bodaboda wanaibiwa sana pikipiki kuanzia mida ya saa 5.30 mpaka saa 9.30 usiku baada ya kubaini hicho kitu tukaanza kutoa elimu kwa madereva ikiwa ni ya kuwatahadharisha kutofanya kazi usiku.

"Tulipita vituo kwa vituo tukaanza kutoa elimu wengi walielewa lakini wachache bado wanakaidi ukishafanya kazi mpaka saa mbili ya usiku inatosha.

"Ukienda kulala mapema, unawanyima wezi nafasi ya kukuibia chombo chako na mwisho wa siku unabaki salama bila tatizo lolote kwa hiyo tulitoa elimu na tukawapa madhara yake ya kufanya kazi mpaka usiku.

"Kwa sababu abiria kama ni jambazi anaweza kumfanya bodaboda chochote hasa nyakati za usiku kwa sababu abiria anakuwa nyuma kama ana kipande cha nondo je dereva atajuaje ndio maana tumekuwa tukitoa elimu kila siku" anafafanua Kamanda Murilo.

Msuguano na 'Panya Road' una historia ya kudhuru afya zao na za watu wengine, hata askari wenyewe waliokuwa wakiwadhibiti.

**OPERESHENI UHALIFU**

"Tumefanikiwa kudhibiti vikundi vya kihalifu, na ajali kwa kiasi kikubwa lakini msaada mkubwa tumepata kutoka kwa wananchi wenyewe kwa maana ya wasamaria wema.



Silaha walizotumia 'panya road' kufanya uhalifu.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Jumanne Muliro.

"Kwa sababu wenyewe ndio wanawajua wezi na hivyo vikundi vilikuwa vinaishi kwenye jamii kwa hiyo watu walikuwa wanawafahamu.

"Pia, tunapita katika shule kutoa elimu na tumeshazifikia shule nyingi sana, tunawaelimisha madhara ya kujiunga na vikundi vya kihalifu, pamoja na namna ya kujiepusha navyo ili na wao wasije wakaiga tabia hizo.

"Hivyo hivyo, kwenye kupunguza ajali nako tumekuwa tukitoa elimu kila siku kwa madereva, lakini Rais Dk Samia (Samia Suluhu Hassan), alisema tuwaonyeshe kwa vitendo waone mtu asipofunga mkanda ajali ikitokea anavyo chomoka kwenye gari anaenda kujibamiza huko.

"Waone mtu akiendesha gari akiwa amelewa anavyokufa bila kujizuia, waone madhara gani mtu anayapata 'anavyo- over take' gari kwenye kona.

"Hiyo pengine itasaidia kuwafanya madereva waogope kwa kuwa watakuwa wameona madhara watakayopata wakienda kinyume na sharia."

"Kitu kikubwa askari wa usalama barabarani ni kusimama imara kwa kusimamia sheria za barabarani bila kujali nani wala nani hiyo ndio misingi yetu kwenye kupambana na matukio hayo." anaeleza Kamanda Muliro.

# Ulaya kuwapima UVIKO – 19 abiria wote watokao China

Mataifa ya Umoja wa Ulaya, yanapanga kutangaza utaratibu wa pamoja utakaotumika kote barani humo katika hatua za kukabiliana na mzozo wa maambukizi ya UVIKO-19 yanayoikumba China.

Mataifa hayo yanazingatia kuweka vizuizi vya safari ambavyo vinaweza kuikasirisha China na sekta ya usafiri wa anga duniani.

Mapema Jumatano, Tim McPhie, Msemaji wa Kamishna wa Umoja wa Ulaya anayehusika na masuala ya Afya, Stella Kyriakides, amesema nchi nyingi za umoja huo zinaunga mkono hatua ya kuweka masharti ya kuwapima kwa lazima abiria kutoka China virusi vya corona kabla ya kuondoka.

"Mazungumzo ya leo yataangazia hali ya mlipuko na yatalenga kuweka msimamo wa pamoja wa Umoja wa Ulaya kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa. Sasa hatua hizi zinalingana na zile zilizowekwa na Kamishna Kyriakides, katika barua ambayo aliwatumia mawaziri wa afya baada ya mkutano wa Desemba 29," alifafanua McPhie.




Ndege ya Shirika la Ndege China. **PICHA: MTANDAO.**

China tayari imekosoa vikali vizuizi vya usafiri ambavyo baadhi ya nchi za Umoja wa Ulaya imeanza kuviweka, na imeonya itachukua hatua za kukabiliana navyo katika siku zijazo. Serikali ya China na wataalamu wa afya wa Umoja wa Ulaya wamesema hakuna haja kubwa ya kuweka vikwazo vyovyote vya usafiri kwa kuwa aina ya virusi vya corona vinavyoibuka kutoka China, tayari vimeenea Ulaya.

Juzi Chama cha Kimataifa cha Usafiri wa Anga, (IATA) ambacho kinajumuisha mashirika 300 ya ndege duniani kote, kimeelezea kupinga hatua ya kuwekwa vizuizi vya usafiri wa anga.

Mkurugenzi Mkuu wa IATA, Willie Walsh amesema utafiti uliofanywa kuhusu kirusi aina ya Omicron unahitimisha kwamba kuweka vizuizi katika usafiri wa anga hakutoleta tofauti yoyote katika kuzuia kuenea kwa maambukizi.

Msemaji wa Serikali ya China, Mao Ning amesema leo kuwa wana matumaini kwamba pande zote zitazingatia kupambana na janga lenyewe, na kuepuka siasa za UVIKO-19.

Hata hivyo, bado Umoja wa Ulaya umeonyesha dhamira yake ya kuchukua hatua za pamoja kuhakikisha abiria wanaoingia kutoka China hawawezi kwa namna yoyote ile kusambaza virusi vipya barani humo. Sweden, ambayo ndiyo inashikilia urais wa Umoja wa Ulaya kwa sasa, imesema wasafiri kutoka China wanahitaji kujiandaa kwa uamuzi utakaochukuliwa katika muda mfupi.

Pamoja na kupima virusi vya corona kabla ya kusafiri, mataifa ya Umoja wa Ulaya, huenda yakakubaliana kuhusu upimaji maalum wa maji machafu katika ndege zinazoingia kutoka China, kuona iwapo yana aina hatari ya virusi ambavyo bado sio vya kawaida katika bara la Ulaya.

Italia ilikuwa nchi ya kwanza mwanachama wa Umoja wa Ulaya kuhitaji vipimo vya virusi vya corona kwa abiria wa ndege wanaoingia kutoka China, pia Ufaransa na Uhispania zilifuata mara moja hatua kama hizo.


***Kwa mujibu wa vyombo vya kimataifa.***

## CHEMSHABONGO NA -00 40 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Mke wa mfalme
5. hueneza Malaria
6. Mji mkuu wa Eritrea
8. Bustani ya Mungu
11. kitu cha kushangaza
12. alikuwa waziri wa mambo ya nje awamu ya nne
14. hekima
16. njiwa
17. kawaida ya kufanya jambo


Chini:
1. Mtu anayefanya kazi ya kutafsiri lugha ya kigeni
2. Mji mkuu wa Togo
3. Tunu
4. sala
7. heshima
8. rudisha
10. kifungu cha maneno yaliyo kamili
13. mnyama ambaye ni mlinzi
15. chunguza kwa makini



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KALENDA
TABU
TAMAA
ALA, ADA,
NYANYASA
MADA
MUNYU
MENYA
NYAMA
UNYAMA
PASADA
ADAMU : AALI
TUME : LHASA

maoni SMS: 0787 00 97 94




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | R | E | K | A | N | I |
| A | M | A | | | G | | N |
| J | A | N | A | B | A | | G |
| I | N | G | I | A | | | A |
| R | A | I | L | A | | | W |
| A | | | A | D | A | N | A |
| N | I | A | | A | | I | |
| I | | S | A | Y | A | R | I |
| | | A | | E | | A | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | U | N | G | U | | A | |
| B | | Y | | Z | U | M | A |
| U | J | U | Z | I | | B | |
| N | | M | A | M | B | O | |
| I | S | A | K | A | | N | |
| | A | | A | | N | I | A |
| | N | | R | | J | | M |
| W | A | S | I | K | I | V | U |
| | A | | A | | A | | A |





## CCM yampongeza Samia kuruhusu mikutano ya siasa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa CCM Mkoa wa Mbeya wapo tayari sasa kupambana kwenye majukwaa ya kisiasa kuwaelezea wananchi utekelezaji wa ilani ya chama katika kipindi cha mwaka 2020 mpaka 2025.

Alisema ruhusa hiyo itawasaidia pia vyama vya siasa kufanya shughuli zao kwa uhuru lakini kwa kuzingatia sheria na utaratibu wa nchi kama Katiba inavyoelekeza.

Alisema kupitia mikutano hiyo wananchi watafahamu mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na serikali katika kuwaletea maendeleo, kwamba wapo tayari kuyasema vyema mazuri yalivyofanywa.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walisema kuwa waliikumbuka mikutano ya hadhara kwani walikuwa wakipata muda wa kusikiliza sera na utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia mikutano hiyo.

Mkazi wa Mtaa wa Sinde, Justine Ahobokile, alisema kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara kulisababisha wananchi kukosa sehemu ya kuhoji utekelezaji wa miradi mbalimbali.

# Watoto wenye mahitaji maalum wapatiwa msaada wa vifaa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATOTO 200 wenye ulemavu mkoani Mbeya wamepatiwa vifaa visaidizi na Shirika la Kuhudumia Watoto wenye Mahitaji maalum Tanzania (CST) katika kipindi cha miezi mitano.

Mkurugenzi wa Shirika la CST, Noela Msuya, alitoa takwimu hizo jana wakati wa hafla ya ufungaji wa mradi wa kuboresha mazingira jumuishi na salama kwa watoto wote nchini kupitia programu ya "Peleka rafiki zangu wote shuleni".

Alisema mradi huo wa kuboresha mazingira jumuishi na salama kwa watoto ulianza kutelekezwa Agosti mwaka 2022 na kumalizika Desemba kupitia ufadhili wa Ubalozi wa Ujerumani.

Alisema vifaa visaidizi na vya ulinzi vilivyotolewa ni miwani, fimbo nyeupe, mafuta kwa watoto wenye ualbino kutoka mikoa mitatu ya mradi.

"Shirika la CST limefikia shule sita za msingi kupitia mradi huu kwa mikoa ya Mbeya, Rukwa na Dodoma kwa kuwajengea uwezo, uelewa na utashi katika utoaji na usimamiwaji wa elimu jumuishi na ulinzi kwa watoto wenye ulemavu," alisema Noela.

Alisema lengo kuu la mradi huo ni kuboresha maisha ya watoto wenye mahitaji maalum hasa wenye ualbino na wenye ulemavu wa kuona na kwamba ubalozi wa ujerumani iliwapatia Sh.milioni 226 kutekeleza mradi huo.

Alisema miongoni mwa mambo wanayojivunia kwenye utekelezaji wa mradi huo ni uhamasishaji wa kitaifa kwa Bunge la Tanzania kwenye masuala ya watoto wenye ulemavu sambamba na uhamasishaji wa haki, ulinzi na usalama wa watoto kwa mikoa nane nchini.

Katika kipindi cha miezi mitano ya utekelezaji wa mradi huo tumefanikiwa ushiriki wa ulinzi na usalama wa watoto kwa kuwafikia wazazi zaidi ya 50 na kufungua klabu za watoto kupigania 51 pamoja na walimu 600 kupatiwa mafunzo ya elimu Jumuishi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliwahakikishia wadau wa elimu kuwa wamedhamiria kutoa suluhu ikiwamo utambuzi na usajili wa watoto hao kwenye mfumo rasmi wa elimu na wa takwimu ili wapate haki zao kama vile huduma mbalimbali za jamii.

Alisema wataendelea kuwatambua, kuwabaini na kuwalinda watoto wote hasa wenye mahitaji maalum ili kujenga taifa lenye usawa, usalama na jumuishi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa Shirika la CST miaka 15 iliyopita watoto wenye ulemavu wamenufaika kwa masuala mbalimbali ikiwamo kujengewa uwezo na maarifa ambayo yamewasaidia kujitegemea.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mradi huo, Damas Mwambije alisema wanajivunia kuwa sehemu ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum ili waweze kutimiza ndoto zao kupitia elimu.

Hata hivyo aliuomba Ubalozi wa Ujerumani kufadhili tena mradi huo ili kuweza kukamilisha mambo ambayo bado hakuyafanya kwa kiwango walichokikusudia.

Akizungumzia faida za mradi huo, Mwalimu kutoka Shule ya Msingi Buigiri iliyoko mkoani Dodoma alisema elimu jumuishi imewasaidia kuwahudumia watoto wa aina zote kwa wakati mmoja.

Alisema elimu hiyo imesaidia kuwahudumia watoto wote bila kujali aina ya ulemavu walionao au kufundishwa kwa mbinu sawa ambazo zimewasaidia kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Aidha, alisema wamejifunza namna ya kuwalinda watoto wenye ulemavu, kuwafundisha namna ya kulinda ulinzi na usalama wao ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile ubakaji, ulawiti na vipigo.



Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (katikati), akizindua shughuli ya ujazilizaji umeme wa Wakala wa Usambazaji wa nishati hiyo Vijijini (REA) jana eneo la Mtakuja Kata ya Iganjo jijini Mbeya. Mradi huo utanufaisha vitongoji na vijiji zaidi ya 3,000 mkoani Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC aiagiza kamati ya ulinzi kusimamia ujenzi madarasa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameziagiza kamati za ulinzi na usalama za wilaya kusimamia maendeleo ya ujenzi wa madarasa kwa kuhakikisha thamani ya fedha inayotumika kwenye ujenzi wa madarasa.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa madarasa kwenye Shule ya Sekondari Msasani iliyoko Mji wa Tukuyu wilayani Rungwe.

Alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo, umegharimu Sh. milioni 400 kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na kuwawezesha watoto wote waliochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza kuanza masomo kwa muda uliopangwa.

"Serikali imetoa fedha lukuki kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mkoani Mbeya, lengo la fedha hizo ni kuwasaidia watoto kusoma kwa utulivu bila kikwazo kinachohusiana na uhaba wa vyumba vya madarasa, nawaomba kamati ya ulinzi na usalama mtusaidie kusimamia kikamilifu fedha hizo ili gharama za fedha ziendane ujenzi wa vyumba vya madarasa," alisema Homera.

Aidha, katika ukaguzi wa ujenzi wa madarasa Sekondari ya Msasani alibaini upungufu katika ujenzi ikiwamo uwekaji wa marumaru katika baadhi ya majengo kutoridhisha. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alimhakikisha Juma Homera kufanyia kazi upungufu wote ulioonekana kwenye ujenzi huo. Alisema kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama watahakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa wilayani Rungwe unakamilisha kwa wakati na kukidhi vigezo vyote vinavyohitajika.

Aliongeza kuwa ujenzi wa madarasa umefikia asilimia 100 na kwamba vyumba 20 vyenye thamani ya Sh. milioni 400 imetumika kukamilisha. Alisema wamepatiwa madawati 500 kwa ajili ya watoto wa kidato cha kuanza ambao wanatarajiwa kuanza masomo Januari 9 mwaka huu.







Mwananchi ambaye jina lake halikupatika akiswaga ng'ombe kwenye barabara kuu ya Dodoma Kondoa juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vyama vya siasa vyatakiwa kutumia mikutano kwa misingi ya demokrasia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BAADA ya serikali kuondoa zuio la vyama vya siasa nchini kufanya mikutano ya hadhara Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma limevitaka vyama vya siasa kuitumia fursa hiyo kwa misingi ya kidemokrasia na siyo kwa maslahi binafsi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan kuruhurusu mikutano hiyo nchini.

Shekhe Mustapha alivitaka vyama vya siasa kutumia fursa hiyo iliyotolewa na serikali kwa faida ya demokrasia kwa maslahi ya taifa na Watanzania bila kujali itikadi zao. Alisema fursa hiyo isitumike kwa mifarakano na chuki baina ya vyama vya upinzani pamoja na kilichopo madarakani.

"Kwanza sisi kama Baraza Kuu la Waisalamu Mkoa wa Dodoma tuna kila sababu ya kumpongera Rais Samia Suluhu Hassa kutokana na hatua hii ya kukaa meza moja na vyama hivyo vya kisiasa na kuweza kutoa uhuru huo wa kufanya mikutano.

"Hivyo ni imani yetu kwa Watanzania walio wengi tutashuhudia kwenye mikutano hiyo vyama hivyo kupitia viongozi wake watatoa hoja ambazo zitakazochochea kukua kwa uchumi kwa maslahi ya Watanzania na siyo kuchochea uvunjifu wa amani tuliyonayo,"alisema.

Shekhe huyo alisema kuwa uhuru uliotolewa usiwe wa kuvunja amani na matusi kwakuwa hali hiyo itaondoa maana halisi iliyokuwepo kwa Rais.

Alisema vyama hivyo vinatakiwa kutoa sera ambazo zitaleta na kuibua upungufu uliopo serikalini.

Aidha, alivishauri vyama kuheshimu chama kilichopo madarakani kwakuwa ndicho kilichopewa ridhaa ya kuongoza dora.

Kadhalika, alivitaka vihakikishe vinashiriki kikamilifu shughuli za maendeleo kwa ajili ya maslahi mapana ya maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, alisema vyama vya siasa vinatakiwa kushirikiana, kusikiliza na kutoa ushauri kwa njia ya hekima na busara na kutoa misaada mbalimbali pale panapohitaji ili kuimarika demokrasia na uchumi.

# Kampuni za bima kuanza kuwalipa majeruhi wa ajali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), inatarajia kukutana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TILA), kwa ajili ya kuzungumzia suala la ulipaji bima ya majeruhi wa ajali na marehemu pale zinapotokea katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi wa LATRA, Habibu Suluo, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari akibainisha kwamba majeruhi au marehemu wanapaswa kulipwa bima za ajali kwa sababu sheria inaruhusu lakini cha kushangaza kampuni za bima hazifanyi hivyo.

Kutokana na hilo alisema wanatarajia kukaa na TILA ili kuhakikisha suala hilo linatendeka ili kila mmoja apate haki ya msingi pale anapopata ajali.

"Tunatarajia kukutana na TILA ili kuwaweka sawa wamiliki wa mabasi kujua nini wanatakiwa kufanya pale ajali zinapotokea,"alisema Suluo.

Alisema wakishakutana watatoa taarifa hiyo kwa jamii ili kuhakikisha kila mmoja analitambua sula hilo.

Suluo alisema wamekuwa wakipigia kelele suala hilo lakini wameona halitekelezwi, ndio maana wameamua kukaa kikao ili kuwekeana mikakati ya kuhakikisha kila mmoja anajua sheria hiyo.

Akizungumzia kuhusu tiketi aliwataka wananchi kuhakikisha wanapewa tiketi ambazo zina majina kamili pamoja na namba za simu.

Alisema kwa kuwa TILA ndiyo wahusika wakuu wa usimamizi wa masuala ya bima, ndiyo maana wanakutana nao ili kuhakikisha wanaliweka sawa suala hilo ili jamii waweze kupata haki yao.

Alifafanua kuwa lengo ni kuona wamiliki wa vyombo vya moto wanakuwa na utaratibu wa kushughulikia bima za ajali kwa abiria.

Alisema kila tiketi anayopewa abiria anapaswa kuikagua ili kuona kama kila kitu kiko sawa ndipo aipokee na kuanza safari. Alisema wanafanya hivyo ili kuhakikisha abiria wote wanakuwa na tiketi kila wanaposafiri ili tatizo linapotokea waweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka.

# Teknolojia mbadala yaanza kutumika ujenzi barabara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umeanza matumizi ya teknolojia mbadala katika ujenzi wa barabara ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi na kuhakikisha kuwa zinadumu kwa muda mrefu bila matengenezo makubwa.

Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu Mkoa wa Dodoma, Happiness Mgalula, alisema hayo juzi jijini hapo katika kikao cha bodi ya barabara.

Alisema kupitia wadau wameanza kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia teknolojia mbadala ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi na kuboresha ubora wa barabara kwa kuhakikisha zinadumu kwa muda mrefu bila matengenezo makubwa.

Alisema kuwa miongoni mwa teknolojia ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni Ecoroads ambayo ni teknolojia mbadala inayotumia majani maalum kuboresha udongo ili kuufanya udongo uwe na uwezo mkubwa wa kuhimili uzito na kudumu kwa muda mrefu.

"Fomula ya kioevu ya Ecoroads inafanya udongo kuwa mgumu na imara hivyo kupunguza matumizi ya kokoto katika ujenzi wa barabara kwa kutumia tabaka moja tu."alisema.

Aidha, teknolojia hiyo ipo katika hatua za utekezaji katika mradi wa majaribio wa Barabara ya Ilazo yenye urefu wa kilometa moja katika Jiji la Dodoma unaotekelezwa na Mkandarasi Asabh Company Limited chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabarani Mijini na Vijijini (TARURA).

Mradi mwingine wa majaribio unatarajiwa kufanyika katika Wilaya ya Chamwino katika Barabara ya Karume Abeid (0.7Km), Rashid Kawawa (1.9Km), Robina (0.65), Malecela (1.72Km) na Mnadani-Mshikamano (1Km) mradi huo upo katika hatua za mwisho za usanifu.

Alitaja teknolojia nyingine kuwa ni Polymer ambayo ni teknolojia mbadala inayotumia polima ili kuboresha udongo uwe na uwezo mkubwa wa kuhimili uzito na kupunguza vumbi kwenye barabara za changarawe.

Teknolojia hiyo imetekelezwa kwenye miradi ya majaribio ya Barabara ya Ndugai iliyopo katika Wilaya ya Dodoma mjini.

Aidha, Mkoa wa Dodoma umewasilisha andiko la mradi husika TAMISEMI kuhusiana na matumizi ya polymer katika ujenzi wa barabara za lami zilizo katika hali mbaya, barabara zote za changarawe na udongo zilizopo mkoani hapo.

"Ili kufanikisha adhma ya kutumia teknolojia hiyo, tumewasilisha majina ya mafundi kwa baadhi ya wilaya ambao watapatiwa mafunzo maalum ya ujenzi wa daraja kwa kutumia mawe katika Mkoa wa Kigoma na wanatarajia kuwatumia mafundi hao katika ujenzi wa madaraja,"alisema.

Alisema kuna tatizo la matumizi mabaya ya barabara kama ujenzi holela ndani ya hifadhi za barabara na upitishaji wa mifugo katika barabara zenye tabaka za udongo, changarawe na wakandarasi kutokuwa na uadilifu na weledi wa kazi.








Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amaan Abed Karume, akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa Tamasha la Tisa la Biashara linalofanyika katika Viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar, ikiwa ni shamrashamra za Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jeshi la Polisi latakiwa kufanya kazi kwa kujitolea, bidii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amelitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa uadilifu, ushirikiano na kujitolea katika kusimamia kesi za waathirika wa matendo ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ili kuyatokomeza.

Alitoa rai hiyo jana katika hafla ya ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kwa watendaji wa huduma ya mkono kwa mkono na madawati.

Waziri Pembe aliwataka maofisa hao kushiriki kikamilifu katika kuzipokea taarifa na kuzifanyia kazi ili kufikia malengo ya kutokomeza ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini.

Aidha, alisema kuwa mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kutatua matatizo ya kesi zinazowakabili waathirika wa udhalilishaji kwa njia ya mkono kwa mkono ili kupata haki zao.

Alisema kuwa wizara imeandaa mpango kazi wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Mtoto ya Mwaka 2011 pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2018 kwa ajili ya kutokomeza vitendo hivyo kwa wanawake na watoto nchini.

Alisema ushirikiano na Jeshi la Polisi na wadau wengine ili kufanya kazi kwa pamoja ili kutokomeza matendo ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia nchini.

Aidha, aliwataka maofisa hao wa polisi kujiepusha na vitendo vya kupokea rushwa ambavyo vitapelekea kutia dosari kwa jamii taasisi husika.

Aliwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kutoa taarifa mapema mara tu yanapotokea matendo hayo ya udhalilishaji nchini.

Waziri Pembe alimpongeza Kamishna wa Polisi wa Zanzibar kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kuunga mkono Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto katika harakati za mapambano ya kutokomeza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Naye Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa utendaji wa kazi kwa watendaji wa huduma za mkono kwa mkono na dawati la jinsia.

Aidha, aliwataka kuwa wawajibikaji na waaminifu, maofisa ambao wamechaguliwa kufanya kazi katika hospitali mpya ambazo zinazotarajiwa kufunguliwa na kufanya kazi nchini.

# Madaktari watakiwa kuwa waadilifu wanapokuwa kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Masoud Ali Mohammed, amewataka madaktari wa hospitali visiwani Zanzibar kuwa waadilifu katika kutekeleza kazi zao za kuwahudumia wananchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika Jengo la Maradhi ya Dharura na Maabara katika Hospitali ya Makunduchi.

Alisema kuwa dhana ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo ya huduma bora ya matibabu ili kuepukana na maradhi ambayo yanawasumbua wananchi.

Alisema kuwa katika maadhimisho hayo ya Miaka 59 ya Mapinduzi, mambo mengi yamefanyika yakiwa na dhamira ya dhati ya kuwaletea maendeleo wananchi pamoja na kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Fatma Mrisho, alisema Wizara ya Afya itaendelea kuwapatia huduma bora wananchi pamoja na mafunzo kwa wataalamu wake.

Aidha, alisema wataalamu hao watawapatia mafunzo pamoja na kuweka vifaa bora, dawa na huduma nyingine muhimu.

Hata hivyo alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Health Improvement Project (HIPZ) wanajenga jengo la kisasa kwa huduma ya maabara.

Mkurugenzi wa HIPZ, Simon Kuhoert, alisema zaidi ya Sh. milioni 570 zimetumika kwa ujenzi wa maabara hiyo, kwamba shirika lake litaendelea kushirikiana na serikali kwa kutoa misaada ambayo ni mahitaji ya msingi kwa wagonjwa.

Daktari wa Dhamana wa Hospitali ya Makunduchi, Mohamed Mtumwa Mnyimbi, alitaja baadhi ya matatizo wanayokutana nayo ni uchakavu wa nyumba za madaktari, upungufu wa wafanyakazi, uzio wa hospitali pamoja na ubovu wa barabara.

# SMZ yaanza mkakati kudhibiti athari matukio ya moto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amesema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuhakikisha inakabiliana na majanga ya moto.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar wakati akikabidhi magari mawili mbili kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa shughuli za kukabiliana na majanga ikiwamo ya moto.

Alisema katika siku za hivi karibuni matukio ya majanga ya moto yakijitokeza ikiwamo katika miradi ya ujenzi wa hoteli za kitalii na kusababisha hasara kubwa kwa wawekezaji.

Harusi alisema kuwapo kwa gari mbili za kupambana na majanga ya moto zitasaidia kukabiliana na majanga hayo na kuwahakikishia usalama wananchi na wawekezaji katika miradi yao kuwa salama.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuimarisha sekta ya uwekezaji katika kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwamo moto, kuwapo kwa magari haya zitasaidia kuwa tayari kujikinga na majanga hayo," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum Zanzibar, Issa Ali Mahfoudh, alisema magari hayo yamenunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni sehemu ya mikakati yake ya kukabiliana na majanga ya moto.

Alisema Sh. bilioni 1.7 zimetumika katika kununua magari hayo ambayo ni ya kisasa, yenye uwezo wa kukabiliana na majanga ya moto hata katika maeneo ya nyumba za ghorofa.


Aidha, alisema sera ya Serikali ya Zanzibar ni kuingia katika mageuzi makubwa ya ujenzi wa miradi ya viwanda vikubwa ambapo huduma za zimamoto zinahitaji kuimarishwa kwa kiwango cha kimataifa.

Naye Kamishna Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Zanzibar, Rashid Mzee Abdalla, alitaja uwezo wa magari hayo katika kukabiliana na majanga ya moto.

Alisema magari hayo yanauwezo wa kubeba maji lita 5,000 pamoja na mapovu lita 500.

Aidha, alisema magari hayo yanauwezo wa kupambana na majanga hata katika nyumba za ghorofa 12 kwa kurudisha maji na mapovu katika kukabiliana na athari za moto.

Alisema: "Magari haya ya kupambana na majanga ya moto ni ya kisasa zaidi zikiwa na sifa nyingi katika kushughulikia athari za moto katika njia mbalimbali ikiwamo kutumia maji pamoja na mapovu."



# Wananchi waanza kutumia maji kutoka Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANACHI wa Shelui wilayani Iramba mkoani Singida, wameanza kutumia maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria na kuondokana na matumzi ya maji machafu.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Maji Ziwa Victoria ambao unatoka eneo la Tinde wilayani Shinyanga kwenda Shelui mkoani Singida.

Alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 99 na wananchi wa Shelui wilayani Iramba mkoani Singida tayari wameanza kuyatumia maji hayo. Sanga alisema kwa sasa wamebaki wananchi wa Tinde wilayani Shinyanga ambao wanasubiri usambazaji wa mabomba ili waanze kupata huduma hiyo.

"Nimeridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu wa maji ya Ziwa Victoria ambao umekamilika kwa asilimia 99 na baadhi ya wananchi kwa mfano kule Shelui wilayani Iramba wameanza kutumia maji haya," alisema Mhandisi Sanga.

Alitaja gharama za mradi huo kuwa Sh. bilioni 24.6 na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizo ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama.

Aliwasihi watumishi wa Wizara ya Maji pamoja na mamlaka za maji kuendelea kutunza miundombinu hiyo ya maji pamoja na mazingira ili mradi huo uwe endelevu na kuwahudumia wananchi kwa muda mrefu.

Naye Mhandisi wa Mipango na Ujenzi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Shinyanga (SHUWASA), Wilfred Lameck, alisema mradi huo kwa upande wa Shinyanga, utahudumia wakazi wa Tinde na Didia wapatao 18,000 na sasa wanasubiri kusambaza mabomba ya maji ili kuanza kutoa huduma.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, akikagua tangi la maji wakati wa ziara ya utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Tinde na Shelui. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi ya kiuchumi ya Tril. 2.3/- yaanza kutekelezwa Kagera

**Lilian Lugakingira,** BUKOBA

SERIKALI ya Mkoa wa Kagera inaanza utekelezaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni moja (Sh. trilioni 2.3) katika Kijiji cha Rubafu kilichoko Tarafa ya Bugabo Wilaya ya Bukoba.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa kituo cha umahiri cha utafiti wa ufugaji wa samaki na mradi wa ufugaji wa samaki katika vizimba.

Akizungumza wakati walipotembelea eneo itakapotekelezwa miradi hiyo, Ofisa Biashara na Uwekezaji mkoani Kagera, Issanya Tendega, alisema miradi itafadhiliwa na Chuo Shirikishi cha Nelson Mandela na Shirika la TACT.

Tendega alisema kuwa ujenzi wa kituo cha umahiri cha utafiti wa ufugaji wa samaki, utawezesha uzalisha mbegu bora za samaki pamoja na kuzalisha vyakula vya samaki.

Hivyo, aliwashukuru wananchi wa Kijiji cha Rubafu kilichoko katika mwambao wa Ziwa Victoria kwa kutoa eneo lenye ukubwa wa ekari 50 kwa Chuo cha Nelson Mandela ili kujenga mradi huo.

Alisema eneo hilo limepimwa na linatosha kuweka vizimba 500,000 na kuwataka wananchi kujiunga kwenye vikundi ili kupewa mafunzo ambayo yatawawezesha kunufaika badala ya kukaa kama watazamaji.

"Vizimba hivi haviwezi kuwekwa na wananchi peke yao, ndiyo maana tumekaribisha wawekezaji ili wawekeze kisasa na kwa tija, lakini wananchi wapate uelewa wa kutosha kutoka kwao nao waweze kufanya ufugaji bora na kujiinua kiuchumi," alisema.

Tendega alisema kuwa miradi hiyo imetokana na kuingia makubaliano kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Chuo Shirikishi cha Nelson Mandela pamoja na Shirika la TACT Septemba 2021.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, pamoja na kamati yake ya ulinzi na usalama walitembelea kijiji hicho na kuwaeleza wananchi kuwa miradi hiyo ni matokeo ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Marekani na kushawishi wawekezaji 12 kujitokeza likiwamo Shirika la TACT.

Chalamila alisema kufikia Januari 10, mwaka huu, wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na TACT wataenda ili kukamilisha mipango ya kutelekeza miradi hiyo.

Kwa mujibu wa Tendega, kizimba kimoja cha kufugia samaki kinakadiriwa kuwa na gharama kati ya shilingi milioni nne hadi sita.

# Halmashauri, KACU kuchimba mabwawa 14 kunusuru kilimo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu wilayani Kahama kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika (KACU) wanatarajia kuchimba mabwawa 14 ya maji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mwenyekiti wa KACU, Hamisi Majogoro, aliyabainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akiwasilisha taarifa yake ya namna ya kukabiliana na ukame katika mkutano wa 27 wa chama hicho.

Alisema hatua hiyo inalenga kukabiliana na ukame ambao unatishia kilimo cha mazao ya chakula na biashara katika eneo hilo.

Majogoro alisema mabwawa hayo yatachimbwa katika Kata ya Ulowa, Ubagwe pamoja na Bukomela na utekelezaji wake utaanza Mei mwaka huu ukiwashirikisha uongozi wa serikali za vijiji na kata ili kuonyesha maeneo sahihi ya kuchimba.

Alisema kukosekana kwa mvua za uhakika katika msimu huu kutasababisha kukosekana kwa tumbaku ya kutosha, hali ambayo iliwafanya kuchukua hatua za haraka za kuchimba mabwawa 14 na kati ya hayo 11 yatachimbwa na Halmashauri ya Ushetu.

"Tunachimba mabwawa haya ili tukabiliane na mabadiliko ya tabianchi, mazao tunayolima hususani tumbaku linahitaji mvua ya uhakika na msimu huu tunatarajia kuzalisha kilo milioni 17, hivyo lazima tuchukue hatua za madhubuti kukabiliana na ukame," alisema Majogoro.

Aidha, Majogoro alisema kuna baadhi ya kampuni ziliingia mikataba ya uzalishaji wa tumbaku na wakulima wameanza kuchukua hatua ya kubeba maji katika magari makubwa na kuwapelekea wakulima shambani lengo likiwa ni kuhakikisha wanayafikia malengo waliojiwekea katika uzalishaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Mwalimu Linno Mwageni alisema, halmashauri yake inategemea mapato ya ndani kupitia tumbaku na pamba hivyo, atahakikisha anachimba mabwawa 11 kati ya 14 yanayotarajia kuchimbwa hivi karibuni.

Alisema kwa sasa wanaendelea na utengenezaji na urekebishaji wa barabara kutoka shambani hadi sokoni kwa kiwango cha changarawe ili kumpatia mkulima fursa ya kufikisha sokoni mazao yake.

Mmoja wa wakulima katika eneo hilo, Mariam Bugumba, alisema mabwawa hayo yatasaidia kuokoa mazao shambani hususani tumbaku kwani linahitaji mvua ya kutosha.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwapongeza kwa hatua wanayochukua katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kwamba atahakikisha analisimamia na utekelezaji wake unaanza mapema ili kunusuru mazao shambani na wananchi wanapata chakula cha kutosha na kuondokana na njaa.

# Prince Harry adaiwa kupigwa na kaka yake Prince William

**LONDON, Uingereza**

MWANAMFALME wa Uingereza, Harry amemshutumu kaka yake Prince William kuwa alimshambulia kimwili wakati wa mabishano kuhusu mke wake Meghan.

Kwa mujibu wa gazeti la Guardian, tukio hilo lipo katika kitabu chake cha kumbukumbu kinachoitwa Spare.

Gazeti hilo liliripoti kwamba kitabu hicho kiliweka mabishano kati ya wawili hao kuhusu mke wa Prince Harry, Meghan.

"Alinishika kola, akaukata mkufu wangu, na akaniangusha sakafuni," gazeti la Guardian lilimnukuu Prince Harry akiandika.

Hata hivyo, BBC News haijaona nakala ya Spare.

Waraka huo hautachapishwa hadi Jumanne ijayo, lakini gazeti la Guardian lilisema lilipata nakala huku kukiwa na kile ilichokiita ulinzi mkali wa kabla ya uzinduzi.

Buckingham Palace bado haijajibu kuhusu suala hilo.

Gazeti hilo lilisema kwamba kaka yake alikosoa ndoa yake na Meghan Markle na kwamba Prince William alimtaja kama mtu mgumu, mchafu na mwenye mabavu.

***BBC***



Jeneza la Papa Benedict XVI likitolewa ndani ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro kwa ajili ya mazishi yake yaliyofanyika jana kanisani hapo katika mji wa Vatican. **PICHA: REUTERS**

# Vifaa vya droni za Iran vinatoka Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

IMEBAINIKA kwamba ndege zisizo na rubani za Kamikaze zinazotengenezwa Irani ambazo jeshi la Russia inazitumia kuishambulia Ukraine zimetengenezwa kwa sehemu na kampuni za Marekani.

Kulingana na kituo cha utangazaji cha CNN, msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani, alisema utawala wa nchi hiyo unatathmini uwezekano wa kuanzisha vikwazo vipya vya kuuza nje dhidi ya kampuni zinazosambaza sehemu ya mifumo kwa Iran.

"Tunaangalia hatua zaidi tunazoweza kuchukua katika suala la vikwazo vya usafirishaji ili kukata ufikiaji wa Iran kwa teknolojia ya droni," alisema Watson.

Jeshi la Russia lilianza kutumia ndege zisizo na rubani za Kamikaze dhidi ya Ukraine msimu uliopita.

Katika miji mikuu ya Kyiv na Magharibi walisema kwamba hizo ni ndege za anga zisizo na rubani zilizotengenezwa na Iran za aina ya Shahed.

Iran hapo awali ilikanusha kuwa ilikuwa imekabidhi ndege zisizo na rubani kwa Russia, lakini ikakubali kwamba kundi la ndege kama hizo zilitumwa Russia kabla ya vita na Ukraine.

Kama CNN inavyoandika katika uchunguzi wake, ndege isiyo na rubani ya Shahed-136 ya Iran ilivunjwa katika sehemu 52.

Ilibainika kuwa sehemu 40 zilitolewa na kampuni 13 tofauti za Marekani.

Vifaa vingine 12 vilitengenezwa na kampuni kutoka Canada, Uswizi, Japan, Taiwan na China.

Kulingana na tathmini nyingine ya mtaalamu wa ndege zisizo na rubani za Iran zilizopigwa risasi huko Ukraine, asilimia 82 ya vifaa vyote hutolewa na kampuni zilizoko Marekani.

Wakati huo huo, waandishi wa chapisho hilo hawakupata ushahidi wowote kwamba kampuni yoyote ya utengenezaji inakiuka vikwazo vya Marekani dhidi ya Iran na kwa makusudi kusafirisha sehemu za ndege zisizo na rubani za Iran.

Wataalamu waliiambia CNN kwamba ni vigumu kwa kampuni binafsi kufuatilia ni nani hasa atakuwa mtumiaji wa mwisho wa bidhaa, hasa katika soko la kimataifa.

Wakati huo huo, Iran na Russia zinaunda kampuni maalum za makombora kununua vifaa kwa haraka zaidi kuliko serikali za Magharibi zinavyoweza kuzifuatilia, uchunguzi ulisema.

CNN iliandika kwamba ilituma maombi kwa kampuni zote ambazo mamlaka ya Kiukreni iligundua bidhaa zao katika droni za Iran.

Kampuni sita zilizojibu zilisisitiza kwamba zinalaani matumizi haramu ya bidhaa zao.

***BBC***

# Papa Benedict azikwa kawaida

**VATCAN, Roma**

KWA mara ya kwanza katika historia ya Kanisa Katoliki, papa aliyeko madarakani anaongoza ibada ya mazishi ya mtangulizi wake.

Maelfu ya waombolezaji wamejitokeza mapema jana asubuhi katika viwanja vya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican, kwa ajili ya kuhudhuria mazishi ya mwanateolojia huyo wa Ujerumani.

Kengele ziligongwa na umati wa watu ulipiga makofi wakati jeneza lenye mwili wa Papa Benedict likipitishwa kutoka sehemu lilipokuwa limewekwa ndani ya Kanisa hilo na kulihamishia mbele ya altare iliyo mbele ya viwanja hivyo, huku makardinali waliovalia mavazi mekundu wakitazama.

Papa Mstaafu Benedict XVI, hakuwa tena kiongozi wa kanisa hilo, lakini viongozi mbalimbali duniani, akiwamo Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz na Waziri Mkuu wa Italia Giorgia Meloni, wamehudhuria mazishi yake.

Vatican ilizialika rasmi nchi za Italia na Ujerumani pekee kuhudhuria mazishi hayo na kuzishauri balozi za kigeni kwamba viongozi wengine wowote wanaotaka kuhudhuria, wanaweza kufanya hivyo lakini kwa uwezo wao binafsi.

Kwa mujibu wa Vatican, viongozi wengine waliohudhuria ni Rais wa Poland Andrzej Duda, Waziri Mkuu wa Hungary Viktor Orban, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Czech Petr Fiala na Rais wa Slovenia Natasa Pirc Musar.

Malkia Sofia wa Uhispania na Mfalme Philippe na Malkia Mathilde wa Ubelgiji pia wanahudhuria.

Nchi nyingi zimewakilishwa na mabalozi wao katika makao makuu ya Kanisa Katoliki huko Vatican.

Zaidi ya makardinali 4,000, mapadri na maaskofu walihudhuria mazishi hayo.

Aliyekuwa rais wa baraza la kipapa la kuimarisha umoja wa Kikristo, Mwadhama Walter Kardinali Kasper, alisema kanisa limempoteza mtu muhimu sana.

"Tumempoteza mtu muhimu sana ambaye pia ameacha alama muhimu katika historia ya Kanisa Katoliki, kwanza kutokana na tabia yake, fadhili na tabasamu, lakini maandiko yake ya theolojia na kiroho," alisema Kasper.

Kwa mujibu wa taarifa za awali za Vatican, mazishi ya Benedict hayakuwa na shughuli kubwa sana, kwa lengo la kuenzi matakwa yake ya kuwa na mazishi ya kawaida.

Mwili wa Benedict utazikwa katika kaburi ambalo mwili wa Papa John Paul II ulizikwa kabla ya kuhamishwa kwa ajili ya kutangazwa kuwa mwenye heri mwaka 2011. Makaburi hayo ya kipapa yako chini ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican.

***DW***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT




**JULIETH SABAS SWAI** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba **TAE 494889** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi **(UHAMIAJI) TEMEKE DAR ES SALAAM mwaka 2022,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/6893/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI




**DIANA STIVINI NGOTI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.1597-0006** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MBOKOMU SEKONDARY mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/4486/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ESTER HERI MFANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S0489-0007** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SUJI SEKONDARY November, 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/8190/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SOPHIA GEOFREY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1011-0071** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Chang'ombe Secondary October 2009. Cheti cha Chuo cha Ualimu chenye namba **E 0577-0082** cha Ebonite Teacher's College May 2013. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NYA/RB/496427/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MARYAM SEIF HEMED** anatangaza kupotelewa na vyeti, cheti cha form four chenye index No. **S0298-0027** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **FEZA GIRLS' SOCONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti cha form six Index No. **S298-0535** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **FEZA GIRLS'SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020 Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/4292/2023.**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AMACHA CREDIT(T)LTD sisi Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara,vitu mbalimbali vya kutumika nyumbani kama vile: Vitanda, Magodoro, masofa, majokofu, Tv, mitungi ya gesi, feni, makabati, cherehani, pasi, meza,

Mnada utafanyika Tarehe 14/01/2023, katika ofisi za **AMACHA CREDIT (T) LTD** zilizopo kigogo Luhamga kuanzia saa nne asubuhi.

**MASHART YA MNADA**
Mteja atatakiwa kulipia bidhaa papo hapo,nathamani itauzwa kama ilivyo,Ukaguzi utaanza Tarehe 06/01/2023

**Mawasiliano piga: -**
**0715-683777/0782548337**
**info@sepcoauctioneering.co.tz**
**www.sepcoauctioneering.co.tz**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ALEX SHUSHU NYANDA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SINORAY YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 171 CYU** YENYE ENGINE No. **SR 156FMI 21058371,** CHASES No. **LD3PCJ6J5M2008371** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI
**GEI/MBO/RB/4515/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI SALUM BUGARU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 363 CJD – TOYOTA NOAH.** Chassis namba SR **500079178.** Engine namba **3S 7979887.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/90/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NA.69/2022**

**KEVIN PONERA ––––– MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SHABAN KOMBA––––– MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi anataarifiwa kuwa Muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 25/01/2023 saa 2:00 asubuhi.
Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/01/2023.

**FORM58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE NO.115b OF 2022 in the matter of the estate of the late FREDRICK FRANK MROPE and in the matter of application for letters of administration by BEATRICE FREDRICK MROPE**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 05 day of 01/2023.
Dated at DAR ES SALAAM this 15 day of 12/2022.

Senior Resident Magistrate

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## DRAKE ATHIBITISHA KUKAMATWA NA BANGI



BAADA ya wasimamizi wake kukanusha, rapa Drake alikamatwa nchini Sweden kwa makosa yanahusiana na matumizi ya bangi, sasa yeye mwenyewe ameonekana kuthibitisha tukio hilo.

Julai mwaka 2022 taarifa zilitoka na kudai Drake anashikiliwa na polisi nchini Sweden kwa makosa yanayohusiana na bangi, wakati akijirusha kwenye klabu moja ya usiku.

Uongozi wa Drake haraka uliibuka na kusafisha hali ya hewa kwa kukanusha taarifa hizo hazina ukweli wowote.

Sasa baada ya miezi mitano, Drake mwenyewe ni kama amethibitisha ilikuwa ni kweli.

Kupitia video ambayo ameiweka instagram, inamwonyesha akiwa chini ya ulinzi wa polisi akiingizwa kwenye gari.

Na pia ameweka mstari kwenye wimbo wake mpya uitwao "Middle of the Ocean".

## ANJELLA AAGA RASMI KONDE MUSIC



MSANII wa bongofleva, Anjella baada ya kimya cha muda mrefu kuhusu mustakabali wake, hatimaye ametoa tamko lake kuhusu kuondoka katika lebo ya Konde Music Worldwide.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Anjella ametoa tamko la kuaga mashabiki na wafuasi wa lebo hiyo inayomilikiwa na msanii Harmonize na kutoa shukrani kwa kushikwa mkono katika kipindi kile ambacho alipata kufanya kazi chini yao.

"Kwaheri Konde Gang na ahsante," aliandika Anjella kwenye picha ya nembo ya lebo ya Konde Music Worldwide.

Tamko lake rasmi linathibitisha msanii huyo amemalizana kila kitu katika mgogoro wa ndani uliohusisha kutamatishwa kwa mkataba wake pamoja na hakimiliki za akaunti zake za mitandao ya kijamii pamoja na nyimbo ambazo alirekodi akiwa chini ya lebo ya Harmonize kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Mwanzoni mwa Novemba mwaka jana, Harmonize alidhibitisha mkataba wa Anjella katika lebo hiyo ulikuwa umetamatishwa na kukanusha madai walikuwa wameshikilia akaunti zake pamoja na hakimiliki za kazi za muziki.

Harmonize alitoa wito kwa yeyote ambaye alikuwa anataka kuendelea kumsaidia Anjella kufanya hivyo.

# HARMONIZE
## AMWANIKA MPENZI MPYA

NYOTA wa muziki wa bongofleva, Rajab Kahali maarafu Harmonize amedokeza mahusiano mapya takriban mwezi mmoja tu baada ya kuachana na Kajala Masanja.

Alhamisi asubuhi, Harmonize alidokeza amezama kwenye dimbwi la mahaba na mwimbaji mwenzake, Feza Kessy.

Bosi huyo wa lebo ya Konde Music Worldwide alichapisha picha kadhaa zinazomwonyesha akiwa na Feza ufukweni mwa bahari na kuambatanisha na ujumbe uliofichwa ukidokeza wawili hao wanachumbiana.

"No mara waaa!!! @fezakessy," aliandika chini ya picha hizo ambazo alichapisha kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Harmonize pia alichapisha video yao fupi ambayo inawaonyesha wakifurahia muda pamoja ndani ya nyumba, wawili hao walionekana kustarehe na wenye furaha kubwa kwa kuwa pamoja.

"Mapenzi ni kamari," aliandika chini ya video hiyo.

Muigizaji Kajala alitangaza kutengana na Harmonize mwishoni mwa mwaka jana baada ya wawili hao kuchumbiana kwa miezi michache. Walikuwa wamerudiana Mei 2022 baada ya Harmonize kuomba msamaha.



HABARI MICHEZO

# DODOMA JIJI YAPIGA HODI SIMBA, YANGA, AZAM FC

**Na Saada Akida, Zanzibar**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC umeziandikia barua rasmi klabu za Simba, Yanga na Azam FC ili kuwaomba kuwasajili kwa mkopo baadhi ya wachezaji wao kwa lengo la kuimarisha kikosi chao kinachoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Uamuzi huo umetokana na ripoti kutoka katika benchi la ufundi la Dodoma Jiji ambalo limeweka wazi wanahitaji viungo washambuliaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Johnson Fortunatus, alisema wanaamini klabu hizo zitawapa majibu chanya ya maombi yao ili kuwasaidia kuingia raundi ya 20 wakiwa imara.

Fortunatus alisema mbali na kuomba wachezaji kwa mkopo, lakini wanajiandaa kufanya usajili wa wachezaji wapya zaidi ya wawili kwa kuwapa mkataba wa kudumu.

"Ni kweli tumepeleka barua ya kuomba wachezaji kwa mkopo hasa nafasi ya kiungo mshambuliaji, moja timu hizo kama tunaweza kupata kuhusu nafasi nyingine tayari kuna wachezaji ambao tuko nao ndani ya timu na wanatakiwa kupewa nafasi na kuaminiwa," alisema Fortunatus.

Kiongozi huyo alisema msimu huu umekuwa na ushindani zaidi lakini bado hawajakata tamaa na wanaendelea kujiimarisha ili kufikia malengo.

"Tunaendelea kusubiri majibu kutoka kwenye timu hizo, kama tutapata nyota ambao tumeomba, tunahakika mambo yatabadilika, tutakuwa na kikosi chenye kujiamini, kikubwa ni kuongeza utulivu," kiongozi huyo alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Dodoma Jiji yenye pointi 21 iko katika nafasi ya 12 wakati timu tatu zilizoko chini ni Coastal Union, Ruvu Shooting na Polisi Tanzania. Dodoma Jiji itasafiri kuifuata Geita Gold FC katika mechi ya raundi ya 20 itakayochezwa Januari 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.

Baada ya mchezo huo, Walima Zabibu hao watarejea nyumbani kuwasubiri Simba katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa Januari 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Oppa Clement (kushoto), akipambana kumtoka kiungo wa Fountain Gate Princess, Stella Kwiligwa katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

# TAFCA Pwani yasimamishwa

**Na Hadija Mngwai**

VIONGOZI wa Chama cha Makocha Mkoa wa Pwani wamesimamishwa kutokana na kosa la kufanya uchaguzi mdogo bila ya kufuata taratibu, imeelezwa.

TAFCA Pwani ilifanya uchaguzi mdogo wa kuziba baadhi ya nafasi za viongozi akiwamo Mwenyekiti, Mweka Hazina na wajumbe wa Kamati ya Utendaji Desemba 28, mwaka jana kwenye Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Kisarawe, mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msajili wa Vyama vya Michezo BMT, Riziki Majala, alisema uchaguzi huo umefanyika kinyume na katiba na sheria ya baraza hilo.

Majala alitaja kosa mojawapo walilofanya ni kujaza nafasi ya viongozi ambao bado walikuwa madarakani hivyo kufanya nafasi moja kuwa na watu wawili.

"Katibu yupo masomoni Chuo cha Michezo Malya, pia nafasi moja ya mjumbe wa kamati ya utendaji imejazwa huku mwenyewe akiwepo. Hivyo tukiwa wasimamizi wa masuala ya michezo nchini tumeliona jambo hili halipo sawa kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa kwetu na kufanyia kazi.

"Kwa mamlaka nilivyokuwa nayo natamka kuusimamisha uongozi wa TAFCA mkoa wa Pwani uliopatikana tarehe 28, kusimamishwa huko kunakwenda sambamba na uchunguzi wa kina na utakapokamilika hatua za kisheria zaidi zitachukuliwa, pia tutatoa taarifa TFF kwa kuwa wao ndio walikuwa wasimamizi katika uchaguzi huu," alisema Majala.

## Simba Queens kusajili mabeki

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Fountain Gate Princess kutoka Dodoma, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema anahitaji kusajili washambuliaji wapya pamoja na kuboresha safu yake ya ulinzi katika dirisha dogo linaloendelea.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Lukula alisema amebaini anahitaji kuongeza nguvu katika idara ya ushambuliaji huku pia amebaini safu yake ya ulinzi haiko imara kama anavyohitaji kuona.

Lukula alisema mechi za ligi hiyo zina ushindani hivyo anataka kuona kikosi chake kinakuwa kamili na imara kwa ajili ya kupambana katika mechi zote.

"Ninatarajia kufanya usajili wa wachezaji wawili, ambao ni mlinzi mmoja pamoja na mshambuliaji, hiyo ni mipango ambayo ninatarajia kuifanya wakati ukifika nitawaeleza wachezaji hao wanatoka nchi gani, ninaomba mashabiki wangu wavute subra," alisema Lukula.

Kocha huyo alisema endapo akifanikiwa kupata wachezaji hao anaamini kikosi chake kitakabiliana na ushindani uliopo katika michezo yote inayowakabili na kufikia malengo ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake ambao wanaushikilia.

Kuhusu mchezo dhidi ya Fountain Gate Princess, Lukula alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu na yenye upinzani mkubwa licha ya kuvuna pointi tatu.

Aliongeza kipindi cha kwanza timu yake ilipoteza umakini na kuzidiwa na wapinzani wao na iliporejea dakika 45 za mwisho iliimarika na hatimaye kuondoka na ushindi.

"Ligi ya msimu huu ni ngumu na kila timu imejipanga vizuri kuhakikisha inapata ushindi katika kila mechi, wapinzani wetu walikuwa vizuri ndio maana kipindi cha kwanza walitudhibiti, binafsi namwombea mchezaji wangu Fatma (Fetty Densa) arejee," Lukula alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate Princess, Alex Alumira, amesema licha ya kupoteza mchezo huo hajakata tamaa na badala yake ataendelea kuonyesha ushindani katika michezo inayofuata.

"Wachezaji wangu wamefanya makosa ambayo yametufanya tupoteze mchezo huu, nitayafanyia kazi makosa hayo ili yasijirudie katika mechi ijayo," alisema Alumira.

## ZISIKUPITE

### JOAO ATAKIWA CHELSEA

MANCHESTER United iko tayari kutoa euro milioni nne ili kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Joao Felix kwa mkopo katika kipindi cha msimu uliosalia, lakini klabu hiyo ya Hispania inataka euro milioni 12 hadi 13 mchezaji wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 22. ***(Relevo)***

### BENFICA YAIBANA CHELSEA

BENFICA imekataa ofa ya kwanza ya Chelsea kwa kiungo wa Argentina, Enzo Fernandez. The Blues wanataka kulipa pauni milioni 112 katika kipindi cha miaka mitatu, lakini klabu hiyo ya Ureno inataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ada yake ilipwe pauni milioni 106 kwa mkupuo mmoja. ***(Mail)***

### MADRID YAPANIA KWA JUDE

REAL Madrid inaamini itashinda mbio za kumnasa kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. ***(Independent)***

### LAMPARD HAKIELEWEKI

KOCHA wa Everton, Frank Lampard atasimamia mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United itakayochezwa leo huku kukiwa na mashaka makubwa kuhusu mustakabali wake wa muda mrefu pale Goodison Park. ***(Guardian)***

### VILLA YAIKATALIA EVERTON

KLABU ya Aston Villa imekataa ombi la Everton kutaka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Danny Ings kwa mkopo. ***(Mail)***

### DOUCOURE ANUKIA FULHAM

EVERTON iko tayari kumruhusu kiungo wa Mali, Abdoulaye Doucoure, mwenye umri wa miaka 30 kuondoka katika klabu hiyo kwa mkataba wa kudumu Januari na mazungumzo yamefanyika na Fulham. ***(Athletic)***

### DONETSK YAIGOMEA ARSENAL

KLABU ya Shakhtar Donetsk inajiandaa kukataa ofa iliyoboreshwa ya Arsenal ya pauni milioni 62 kwa winga wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhailo Mudryk mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### CHELSEA MAMBO SAFI

CHELSEA iko tayari kutoa ofa yoyote ambayo Arsenal itampa, Mykhailo Mudryk ili kuwashinda Arsenal kwenye usajili wake. ***(Independent)***

### FIRMINO ATAJWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino anazivutia klabu za Saudi Arabia, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anategemea kuongeza mkataba wake na Liverpool huku mazungumzo na klabu hiyo yakiendelea. ***(Sky Germany)***

### MARTINEZ ANUKIA BARCA

BARCELONA inatarajiwa kumsajili beki wa Hispania, Inigo Martinez mwenye umri wa miaka 31 msimu wa joto wakati mkataba wake na Athletic Bilbao utakapokamilika. ***(Sport)***

### JACKSON AINGIA SOKONI

KLABU ya Southampton ipo kwenye mazungumzo na kambi ya kiungo wa Villarreal, Nicolas Jackson, kuhusu usajili wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 21 kwa mkopo na chaguo la kumnunua msimu wa joto. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA ANAAMINI ATABAKIA UNITED

Golikipa huyo afunguka yuko katika hatua nzuri ya mazungumzo na klabu hiyo na…

**MANCHESTER, England**

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, amesema ana uhakika mazungumzo kuhusu kusaini mkataba mpya na klabu hiyo yatamalizika kwa njia nzuri.

Mkataba wa De Gea pale Old Trafford unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na United wana chaguo la kuongeza kwa mwaka mwingine.

Vyanzo vya ndani kutoka katika klabu hiyo, vimeiambia ESPN United imechagua kuanza mazungumzo juu ya makubaliano ya muda mrefu.

Lakini ikiwa masharti mapya hayatakubaliwa na United, De Gea anaweza kuondoka bure msimu wa joto, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amebainisha anataka kubaki.

"Nimetulia sana," alisema De Gea baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bournemouth katika mechi iliyochezwa.

"Nimezingatia tu mazoezi yangu na nitafanya vyema kadri niwezavyo. Lakini, kwa hakika mazungumzo yataisha kwa njia nzuri tu."

De Gea ameichezea United zaidi ya mechi 500 tangu atue klabuni hapo akitokea Atletico Madrid mwaka 2011.

Kwa mujibu wa ESPN, United iko kwenye mazungumzo na Jack Butland ili kuwa msaidizi wa De Gea, huku Martin Dubravka akiwa amerejea Newcastle United baada ya mkopo wake wa muda mrefu kupunguzwa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,063,6

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
EVERTON
1 | 1.48
X | 4.08
2 | 6.13

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# FERNANDEZ AZIGONGANISHA CHELSEA, BENFICA

**LONDON, England**

CHELSEA na Benfica bado ziko katika mazungumzo juu ya kile ambacho kinaweza kugeuka kuwa ada ya uhamisho wa rekodi nchini England kwa kiungo wa Argentina, Enzo Fernandez, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ana nia ya kutaka kuhamia Stamford Bridge na Benfica wako tayari kukubaliana na uhamisho huo iwapo kipengele chao cha kuachiliwa kwa euro milioni 120 kitatimizwa kikamilifu.

Mazungumzo yanaendelea huku kukiwa na ujumbe unaotofautiana kutoka katika vyanzo vilivyo karibu na klabu hizo mbili.

Wale walio karibu na Benfica wanasema Chelsea wamedai wanaweza kulipa hadi euro milioni 127, huku wakitaka kuishawishi klabu hiyo ya Ureno ikubali malipo ya awamu.

Hata hivyo, vyanzo kutoka ndani ya Chelsea vinasisitiza bado hawajafikia makubaliano ya kulipa kiasi hicho na wanatumainu kufanya mazungumzo na Benfica kwa kiwango cha chini zaidi.

Rekodi ya uhamisho wa Ligi Kuu England ni pauni milioni 100 iliyolipwa na Manchester City kwenda Aston Villa kwa ajili ya kumsajili, Jack Grealish mwaka 2021.

Klabu hiyo inamtumia wakala Jorge Mendes katika juhudi za kufikia makubaliano.

# Xavi: Tunahitaji kuongeza nguvu

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeondoka kwenye mchezo wake wa Copa del Rey dhidi ya Intercity ikiwa haina furaha, kwa mujibu wa kocha Xavi.

Blaugrana ilihitaji bao la muda wa majeruhi kutoka kwa Ansu Fati ili kupata ushindi wa 4-3 dhidi ya timu hiyo ya daraja la tatu, ambao Oriol Soldevila alifunga hat-trick ya ajabu.


Na baada ya mchezo huo, Xavi anafahamu kwamba kuna mengi ya kuboresha kabla ya mechi ngumu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Atletico Madrid wikendi hii.

"Tuliruhusu mengi katika mchezo ambao tulikuwa tumedhibitiwa sana," alisema akiuambia mkutano wa waandishi wa habari baada ya mechi.

"Hatuwezi kuondoka tukiwa na furaha, mchezo ulikuwa mzuri sana, lakini lazima tuongeze nguvu. Katika ulinzi inaweza kutokea, lakini mchezo ulipaswa kumalizika na kumekuwa na ukosefu wa nguvu.

"Lakini tulilazimika kutawala mchezo, na tulikuwa wazuri. Tuna mambo ya kuvutia, lakini tumeteseka sana.

"Leo (juzi) nina furaha na mchezo. Lakini tuko katika wakati mzuri wa kucheza. Ni lazima nifikirie ni nini tunaweza kuboresha."



## HABARI MICHEZO

605,974/-

# IHEFU YATANGAZA KUTEMA WACHEZAJI WAKE WATANO

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA nahodha wa Ihefu SC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, straika, Joseph Kinyozi, ni mmoja kati ya wachezaji watano waliotangazwa kuachwa katika kikosi cha timu hiyo inayopambana kuhakikisha haishuki tena daraja.

Uamuzi huo unalenga kukiimarisha kikosi kwa kupata nafasi ya kusajili wachezaji wapya ambao wataisaidia timu hiyo kupata matokeo chanya.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Ihefu imewataja nyota wengine walioachwa ni pamoja na Omari Hamis, Evaligetus Mujwahuki, Wema Sadoki na Ally Ramadhani 'Oviedo'.

"Klabu inawatakia kila la kheri wachezaji hao kwenye maisha mengine ya soka popote waendapo," ilisema taarifa ya klabu hiyo yenye makazi yake Mbarali, mkoani Mbeya.

Taarifa iliongeza klabu hiyo inahitaji wachezaji wenye viwango vya juu zaidi na hatimaye kufikisha malengo waliyonayo.

Habari zilizopatikana jijini zinasema mabosi wa klabu hiyo wako katika hatua za mwisho za kukamilisha usajili na mchakato huo utakapokamilika watawatangaza nyota hao wapya waliopewa mikataba.

"Wakati wowote kuanzia kesho (leo), klabu inaweza kutangaza wachezaji wapya ambao imewasajili kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo," kilisema chanzo chetu.

Ihefu ndio timu pekee ambayo imeifunga Yanga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na kufanya 'unbeaten' yao kuishia katika mechi ya 49.

Katika msimamo wa ligi hiyo, iko kwenye nafasi ya 13 ikiwa na pointi 20, imeshinda mechi sita, sare mbili na imepoteza michezo 11.



Wachezaji wa Kituo cha Michezo cha Wakati Ujao wakimdhibiti nyota wa timu hiyo, Heri Amri (katikati), katika mchezo wa kusaka kikosi kwa ajili ya kushiriki mashindano mbalimbali yajayo uliofanyika kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ROBERTINHO AWAPA 'TANO'

INATOKA UK. 32

hadi hatua ya mwisho ili kupata matokeo mazuri na kufikia malengo yanayotarajiwa," alisema kocha huyo.

Tayari Mbrazil huyo ameshakabidhi faili la timu ikiwamo taarifa za mchezaji mmoja mmoja na tathimini ya ligi na mechi zilizobakia ili kufikia malengo ya kupata ushindi katika kila mechi.

Robertinho anatarajia kuanza majukumu yake baada ya kikosi kurejea Dar es Salaam na kuingia kambini kwa nyota wote wakiwamo Clatous Chama, Mosses Phiri, Shomari Kapombe na wengine ambao walipewa mapumziko.

Jana usiku Simba ilikuwa inakamilisha ratiba kutokana na kutoweza kufikisha pointi nne ambazo Mlandege FC wanazo hata wakiifunga KVZ.

Ikirejea jijini, Simba itaendelea na maandalizi ya kuikaribisha Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 20 itakayochezwa Januari 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 44 iko katika nafasi ya pili nyuma ya vinara na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 50 kibindoni.

# YANGA, SINGIDA

INATOKA UK. 32

Mapinduzi.

Utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji kulipa kisasi kwa Yanga, kuwafunga katika mchezo wetu huu wa pili kwenye mashindano haya, tunawaheshimu na tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu," alisema Lule.

Bingwa wa michuano hiyo inayochezwa kila mwaka anatarajia kupata zawadi ya Sh. milioni 30.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/01/23 | 18:00 | KAS Eupen vs Royal Charleroi SC | 2.65 | 3.55 | 2.44 |
| 02. 07/01/23 | 18:00 | Millwall FC vs Sheffield United | 2.90 | 3.20 | 2.43 |
| 03. 07/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Burnley FC | 2.32 | 3.40 | 2.90 |
| 04. 07/01/23 | 18:00 | Cambridge United vs Bristol Rovers | 2.85 | 3.30 | 2.41 |
| 05. 07/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Cheltenham Town | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 06. 07/01/23 | 18:30 | RKC Waalwijk vs SC Heerenveen | 2.43 | 3.50 | 2.70 |
| 07. 07/01/23 | 20:30 | Brentford FC vs West Ham United | 2.65 | 3.25 | 2.65 |
| 08. 07/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Go Ahead Eagles | 2.60 | 3.30 | 2.65 |
| 09. 07/01/23 | 22:45 | Royal Antwerp FC vs KAA Gent | 2.44 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 07/01/23 | 23:00 | Espanyol Barcelona vs Girona FC | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 08/01/23 | 14:30 | US Salernitana vs Torino FC | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 12. 08/01/23 | 15:30 | Bristol City vs Swansea City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 13. 08/01/23 | 17:00 | Spezia Calcio vs US Lecce | 2.55 | 3.10 | 2.85 |
| 14. 08/01/23 | 18:00 | SV Zulte Waregem vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.70 | 3.70 | 2.32 |
| 15. 08/01/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.85 | 3.25 | 2.46 |
| 16. 08/01/23 | 18:45 | Excelsior Rotterdam vs FC Groningen | 2.65 | 3.55 | 2.45 |
| 17. 08/01/23 | 19:00 | Fenerbahce Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.39 | 3.50 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 06/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 4196 | Indonesia vs Vietnam | 3.46 | 3.07 | 2.06 |
| 14:30 | 4561 | Perth Glory vs Western Sydney | 3.39 | 3.24 | 2.12 |
| 15:00 | 2038 | AC Milan Youth vs Napoli Youth | 1.77 | 3.84 | 3.65 |
| 16:00 | 1190 | AS Ashdod vs Hapoel Rishon Lezion | 3.61 | 3.16 | 2.10 |
| 16:00 | 1712 | Bnei Yehuda vs Hapoel Ramat Gan | 2.03 | 3.30 | 3.65 |
| 16:00 | 5105 | SC Kfar Qasem vs El Fahem | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 16:00 | 5115 | Green Buffaloes vs FC Muza | 1.97 | 2.97 | 3.90 |
| 16:00 | 5562 | Hapoel Acre vs Nazareth Ilit | 2.06 | 3.25 | 3.60 |
| 17:00 | 1342 | RC Kouba vs ASM Oran | 2.02 | 3.06 | 3.59 |
| 17:00 | 2289 | Fiorentina Youth vs Roma Youth | 3.12 | 3.65 | 1.98 |
| 17:00 | 2390 | Sportive de Sale vs Olympique Dcheira | 2.41 | 2.82 | 3.02 |
| 17:00 | 2964 | Northeast United FC vs Bengaluru FC | 4.29 | 3.61 | 1.70 |
| 17:00 | 4548 | Shabab Al Dhahiriya vs Shabab Alsamu | 2.09 | 3.31 | 3.12 |
| 17:00 | 4577 | Shabab AL Sahel vs Al-Bourj FC | 2.07 | 3.01 | 3.50 |
| 18:15 | 2530 | Ponferradina vs Villarreal B | 2.20 | 3.17 | 3.22 |
| 18:45 | 5447 | Iraq vs Oman | 2.31 | 2.93 | 3.07 |
| 19:00 | 4089 | Sassuolo Youth vs Bologna Youth | 1.76 | 3.80 | 3.70 |
| 20:00 | 1232 | Paris FC vs Valenciennes | 1.89 | 3.53 | 3.82 |
| 20:00 | 2671 | Nea Salamis vs EN Paralimni | 2.02 | 3.35 | 3.60 |
| 20:00 | 3114 | Grenoble Foot vs Nimes | 2.30 | 3.03 | 3.23 |
| 20:00 | 3971 | PAU FC vs Montpellier | 4.17 | 3.58 | 1.80 |
| 20:00 | 5701 | Strasbourg vs Angers | 1.84 | 3.58 | 3.98 |
| 20:15 | 5927 | Difaa El Jadidi vs Olympique Khouribga | 2.07 | 3.02 | 3.51 |
| 20:30 | 1065 | Richards Bay FC vs Mamelodi Sundowns | 5.75 | 3.52 | 1.61 |
| 20:30 | 2119 | Moroka Swallows FC vs Chippa Utd | 2.13 | 2.92 | 3.72 |
| 20:30 | 2522 | Elche vs Celta Vigo | 3.55 | 3.25 | 2.08 |
| 20:30 | 5724 | Sporting Gijon vs Levante | 2.47 | 2.96 | 2.96 |
| 21:30 | 3318 | Yemen vs Saudi Arabia | 9.54 | 4.87 | 1.27 |
| 21:30 | 4652 | Cholet vs Red Star | 3.51 | 3.41 | 1.98 |
| 22:00 | 1066 | Jong AZ Alkmaar vs Heracles Almelo | 3.65 | 3.80 | 1.83 |
| 22:00 | 1452 | NAC Breda vs Jong PSV | 2.17 | 3.41 | 3.01 |
| 22:00 | 1588 | Den Bosch vs Jong Utrecht | 2.05 | 3.50 | 3.21 |
| 22:00 | 2012 | PEC Zwolle vs Almere City | 1.63 | 3.89 | 4.63 |
| 22:00 | 2544 | FC Oss vs Telstar | 3.11 | 3.35 | 2.15 |
| 22:00 | 2794 | VVV Venlo vs Helmond Sport | 1.72 | 3.81 | 4.15 |
| 22:00 | 3493 | Willem II Tilburg vs Roda Kerkrade | 2.09 | 3.40 | 3.20 |
| 22:00 | 3510 | Benfica vs Portimonense | 1.15 | 7.38 | 14.95 |
| 22:00 | 4421 | Twente vs Emmen | 1.47 | 4.26 | 6.14 |
| 22:00 | 4440 | Jong Ajax vs FC Eindhoven | 2.08 | 3.60 | 3.06 |
| 22:00 | 4991 | Maastricht vs De Graafschap | 3.36 | 3.51 | 1.99 |
| 22:00 | 5261 | Dordrecht vs ADO Den Haag | 2.81 | 3.46 | 2.27 |
| 22:30 | 1309 | Briton Ferry vs Trefelin FC | 1.53 | 4.60 | 5.00 |
| 22:30 | 4610 | Raja Casablanca vs Ittihad Tanger | 1.30 | 4.56 | 8.93 |
| 22:45 | 1841 | Standard Liege vs St Truiden | 2.45 | 3.27 | 2.77 |
| 22:45 | 2543 | Raith Rovers vs Dundee FC | 3.16 | 3.26 | 2.16 |
| 22:45 | 3820 | Flint Town United vs Aberystwyth Town | 1.89 | 3.55 | 3.46 |
| 23:00 | 3249 | Valencia vs Cadiz CF | 1.56 | 4.01 | 5.62 |
| 23:00 | 4239 | Manchester Utd vs Everton | 1.48 | 4.08 | 6.13 |
| 23:00 | 5217 | Leganes vs Lugo | 1.70 | 3.36 | 5.14 |
| 23:00 | 5823 | Chateauroux vs Paris St Germain | 27.77 | 8.72 | 1.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Januari 6, 2023
Nipashe



UKURASA 29

## De Gea anaamini atabakia United



Mshambuliaji wa Yanga, Lazarus Kambole (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa KMKM katika mechi ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar juzi usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# ROBERTINHO AWAPA 'TANO' MKUDE, KIBU

●●●Kocha huyo mpya asema hakuna kitakachoshindikana katika vita ya...

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

LICHA ya timu yake kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Mlandege katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani hapa, Kocha mpya wa Simba, Roberto Olivera 'Robertinho', amevutiwa na viwango vya wachezaji wake waliocheza mchezo huo akiwamo kiungo, Jonas Mkude.

Robertinho ametambulishwa rasmi kuwa Kocha Mkuu na juzi alihudhuria mazoezi akimtazama Msaidizi wake, Juma Mgunda, aliyekuwa akikinoa kikosi cha timu hiyo baada ya kuwapo jukwaani Jumanne usiku akishuhudia ikicheza kwa mara ya kwanza.

Mbali na Mkude, wachezaji wengine ambao walimvutia kocha huyo ni pamoja na mshambuliaji, Kibu Denis na beki, Kennedy Juma.

Taarifa zaidi kutoka Simba zinasema kocha huyo amesema anahitaji nyota hao wabakie kikosini hapo na pia amemtaka Mgunda kuwapa muda zaidi katika mechi ya pili dhidi ya KVZ FC iliyotarajiwa kuchezwa jana usiku ili kuwaangalia zaidi.

Taarifa zaidi zinasema Robertinho anapokea ripoti ya kiufundi kutoka kwa mtathimini wa timu hiyo, Kelvin Mavunga ambaye amekuwa kwenye kikosi hicho kwa zaidi ya mwaka sasa.

Hata hivyo katika mazoezi ya juzi, wachezaji Sadio Kanoute, Kibu na golikipa, Beno Kakolanya, walikuwa benchi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho alisema anaimani kubwa na kikosi chake kitafanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao na kubwa kuifikisha Simba katika hatua ya nusu au fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema anafahamu hakuna kazi rahisi kufikia malengo hayo kama wachezaji hawatajituma katika kila mechi wanayocheza.

"Hakuna kinachoshindikana kwa sababu wachezaji wanatakiwa kutambua thamani ya nembo ya klabu, kuitumikia ipasavyo na wanatakiwa kupigania timu

INAENDELEA UK. 31

## Yanga, Singida mechi ya kisasi

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

USHINDI na kisasi ndio neno linalotawala kuelekea ya katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi kati ya Yanga dhidi ya Singida Big Stars itakayochezwa leo kuanzia saa 2:15 usiku kwenye Uwanja wa Amaan.

Timu hizo ziko Kundi B, zikilingana pointi lakini Singida Big Stars wanaongoza kundi hilo kutokana na kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo wake wa kwanza wakati Yanga ilipata ushindi wa goli 1-0.

Wenyeji KMKM inaburuza mkia katika kundi hilo na imeshaondolewa kwenye mashindano hayo ya mwaka huu baada ya kupoteza mechi zote mbili.

Yanga imekuwa na matokeo mazuri inapokutana na Singida Big Stars, iliwafunga mabao 4 -1 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Novemba 17, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema mchezo wa leo unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya kila upande kuufahamu na kuutambua ubora na madhaifu ya mwenzake.

Kaze alisema Singida Big Stars ni timu nzuri na imekuja na wachezaji wake wote muhimu katika michuano hiyo tofauti na wao, lakini wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kusonga mbele.

"Tunawafahamu vizuri Singida Big Stars, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wetu anajua madhaifu na ubora wa mwenzake, kikubwa tunahitaji kupata matokeo mazuri ili kucheza hatua ya nusu fainali," alisema Kaze.

Naye Kocha Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, alisema wamejipanga vizuri na wako tayari kwa mchezo huo ambao malengo yao ni kulipa kisasi kutoka kwa wapinzani wao, Yanga.

Lule alisema wanakumbuka mara ya mwisho walipoteza mechi dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo hawataki hawataki kurudia makosa waliyofanya awali.

"Haya mashindano tofauti kabisa na ligi, tumewaona Yanga walivyocheza na tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kesho (leo), malengo yetu makubwa ni kufika nusu au fainali ya

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042